**9 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

__________

## MAJADILIANO YA BUNGE

__________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 9 Juni, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini na Mbili, leo tarehe 9 Juni, 2025.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Maelezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)*.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025]*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Katibu, tunaendelea.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 533

**Kuwawezesha Kiuchumi Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inawawezesha kiuchumi Watu wenye Ulemavu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha kiuchumi Watu wenye Ulemavu, Serikali imeendelea kufanya yafuatayo: -

(1) Kutoa Mikopo ya 10% isiyokuwa na riba inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo watu wote wenye ulemavu wametengewa asilimia mbili;

(2) Utekelezaji wa takwa la Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 440 la kutenga 30% ya zabuni za umma kwa ajili ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye Ulemavu;

(3) Utekelezaji wa mipango ya maendeleo endelevu ya watu wenye ulemavu na ile ya kibajeti ikiwemo fungu maalum kwa wenye ulemavu;

(4) Kuwapatia elimu itakayowawezesha kushiriki katika shughuli jumuishi za kiuchumi; na

(5) Utekelezaji wa miongozo mbalimbali ukiwemo ule wa matumizi ya teknolojia saidizi ili kuwawezesha nao kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali inaonesha imewezesha maeneo mbalimbali ya kiuchumi kwa watu wenye ulemavu, lakini bado kuna watu wenye ulemavu wengi sana hawaelewi wapi waende wakapate fursa hizo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuongeza elimu kwa watu wenye ulemavu ili waelewe fursa ambazo wanapewa na Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imendelea kufanya kazi kubwa sana ya kutoa elimu, pia kuhamasisha na kuwaunganisha watu wenye ulemavu. Itakumbukwa mwaka 2022

Mheshimiwa Rais alikutana na watu wenye ulemavu pale Chamwino - Ikulu na akawasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo ambayo ni makubwa yalifanyika, kwanza ni kuimarisha Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu ambapo aliwanunulia mpaka kiwanja kwa ajili ya kujenga makao makuu yao kama chombo cha kuwasaidia kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili Mheshimiwa Rais pia kwa maagizo yake mahsusi alitaka kuwepo kwa uwezesho wa ruzuku kupitia Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu hasa kupitia *SHIVYAWATA* zaidi ya shilingi bilioni moja inatengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeendelea kukutana na makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, redio, magazeti pia kukutana nao katika makundi mbalimbali hasa kwenye sekta ambazo wapo watu wenye ulemavu. Kwenye sekta ya sanaa tunao Jumuiya *Band* na bendi nyingine za watu wenye ulemavu ambapo tunawasaidia pia kama Serikali kuweza kujitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye michezo pia *Tembo Warriors* ambayo ni Timu ya Watu Wenye Ulemavu ambapo pia tumeendelea kuonesha kwamba katika hayo maeneo tunawatambua. Kwenye kilimo wapo, wanapewa maeneo kama mpango uliopo kwenye programu za kilimo, madini hata kwenye eneo lingine la watu wenye ulemavu kwenye utoaji wa elimu wameendelea kufikiwa, kwa maana ya kuhamasishwa kwenda kwenye vyuo vya ufundi na marekebisho ya watu wenye ulemavu ambapo kuna vyuo zaidi ya saba ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, Mheshimiwa Rais alitoa zaidi ya shilingi bilioni 3.6 kuvifufua na vimeshaanza kufanya kazi kwenye maeneo mbalimbali, pia tunajenga vyuo vingine vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu na utoaji wa elimu unagusa kila sekta ambapo watu wenye ulemavu wapo na Serikali tumeendelea kufanya hivyo.

Ninaomba pia Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yao waendelee kuiona ofisi hii. Tupo wazi kwa ajili ya kuendelea kusaidia watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na mashirika yote yanayojihusisha na watu wenye ulemavu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patrobas Katambi kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, litaulizwa na Mheshimiwa Mwita Getere.

Na. 534

**Ujenzi Kituo cha Afya Rabour – Rorya**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Rabour - Rorya utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Kituo cha Afya cha Rabour kilipokea jumla ya shilingi milioni 530 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la maabara, jengo la wazazi na jengo la kupasulia wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2025, majengo matatu yamekamilika na huduma za wagonjwa wa nje na maabara zinatolewa. Aidha, jengo la upasuaji na jengo la kufulia ujenzi wake umefikia 80%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenge fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya cha Rabour.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Swali la kwanza, tumekuwa na ujenzi wa vituo vya afya kwenye maeneo mbalimbali, lakini havikamiliki. Kituo cha Afya cha Rabour kimekamilika, lakini sasa hata vitanda tu, hakina. Sasa, ni lini Serikali itapeleka vitanda kwenye kituo hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kituo cha Afya Unyari kimejengwa na wananchi, wamejitahidi sana kujenga *theatre,* lakini mpaka leo hiyo *theatre* bado hakijakamilika na wala hakina vitanda. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba kwenye Kituo cha Unyari na kumaliza hiyo *theatre? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na ujenzi wa vituo vya afya. Ujenzi wa vituo hivi unafanyika kwa awamu. Tulianza na ujenzi wa majengo matano ya awamu ya kwanza, lakini tutakwenda kwenye ujenzi wa majengo yanayosalia awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza ninaomba nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Getere kwamba Serikali inatambua kwamba katika majengo matano ya awamu ya kwanza ya Kituo cha Afya cha Rabour katika Halmashauri ya Rorya, majengo matatu yamekamilika, majengo mawili yapo zaidi ya 80% na tayari Serikali imetenga fedha katika mwaka wa fedha ujao shilingi milioni 226 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukamilishaji wa majengo hayo ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Rorya kuhusiana na vifaatiba na hususan vitanda, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka shilingi 1,150,000,000.00 ndani ya huu mwaka wa fedha na mwaka wa fedha uliopita katika Halmashauri ya Rorya. Fedha hiyo ni fedha nyingi inatosha kununua vitanda na vifaatiba vyote kwa ajili ya vituo vya afya na Hospitali ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rorya kuhakikisha kwamba, fedha hiyo shilingi 1,150,000,000.00 ambayo tayari imepelekwa kwenye Halmashauri yake inunue vitanda na vifaatiba kwa ajili ya kuanza kutoa huduma katika kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na Kituo cha Afya cha Unyari nayo pia katika Halmashauri ya Bunda Serikali ilishapeleka fedha kwa ajili ya vifaatiba. Ni wajibu wa Mkurugenzi, Mganga Mkuu wa Halmashauri na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara kuhakikisha wanaweka kipaumbele kuwasiliana na *MSD* na kupata vifaa hivyo mapema ili wodi hizo zianze kutoa huduma stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Ester nimewaona.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita tulijaza fomu za kupewa vituo vya kimkakati. Jimbo la Kalenga tulijaza katika Kata ya Kihanga. Wiki tatu zilizopita nilipigiwa simu kwamba wamepokea fedha na nikawaelekeza mahali pa Kwenda, lakini juzi ninapigiwa simu na Afisa Mipango kwamba fedha hiyo haikwenda Kalenga. Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha kwenye Kituo cha Afya cha Kihanga na Waziri anaweza kunihakikishia hapa ninaweza kufuatilia na kunipatia majibu kwa nini nilipigiwa na sasa ninaambiwa kinyume chake? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kufuatia maombi ya Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yote 214 kupata vituo vya afya vya kimkakati kwenye Kata ambazo ziliainishwa, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga, Mheshimiwa Kiswaga aliwasilisha Kata ya

Kihanga na tayari Mheshimiwa Rais ametenga fedha kwenye bajeti ya dharura zaidi ya shilingi 53,500,000,000.00 na tayari ameshatoa shilingi 30,000,000,000.00 kwa ajili ya majimbo 120 ya mwanzo awamu ya kwanza na baadaye tutamalizia yale majimbo 94 yanayobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kiswaga kwamba, yale majimbo awamu ya kwanza 120 tayari yameshapokea fedha mpaka wiki iliyopita, lakini Jimbo la Kalenga lipo awamu ya pili na alipigiwa simu kwa sababu walikuwa wanajiridhisha kwamba amependekeza Kata ya Kihanga na Serikali inaendelea kutafuta hiyo fedha iliyobaki kwa ajili ya majimbo yote 94 liliwemo Jimbo la Kalenga kwa maana ya kupelekewa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatekeleza ahadi yake na kazi inaendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, nimekuona.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Bunda tunajenga hospitali yetu, na hii ni mara ya pili, ninaliuliza hili swali humu Bungeni. Kuna shilingi milioni 800 ilikuja ikamezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri anaijua ile hospitali ambayo tunaijenga katika Kata ya *Bunda Store*, sasa hivi ime-*stuck*. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha ili tumalize hospitali yetu ya Halmashauri ya Mji wa Bunda ili wananchi wetu kwenye Halmashauri ya Mji wa Bunda wapate huduma zinazostahili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilipeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda. Ni kweli pia kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya amefuatilia mara kadhaa kwamba tupeleke fedha ile na hasa ile shilingi milioni 800 ambayo

ilirejeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya 2015 baada ya kuvuka 30 Juni, katika huu mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie tu kwamba, fedha ile ambayo ilirejeshwa, Serikali tumeitenga tena kwenye bajeti ya fedha ya 2025/2026, pia tumeongeza fedha kwa sababu tunafahamu shilingi milioni 800 haitatosha kukamilisha yale majengo. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Bulaya kwamba, tunajua umuhimu wa kukamilisha hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda na ndiyo maana fedha zilipelekwa, tumetenga kwenye mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwamba Serikali ni Sikivu, itahakikisha inapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha Hospitali ya Halmashauri ya Mji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege, nilikuona.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Wakati wa ziara ya Waziri Mkuu katika Jimbo la Mwibara mwaka juzi alielekeza kuwa Kituo cha Afya kijengwe Bulamba.

Je, ni lini kituo hicho kitajengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vituo vya afya ambavyo ni ahadi za viongozi wakuu wa Kitaifa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika mipango yetu tunaweka kipaumbele cha hali ya juu katika maeneo hayo ikiwemo katika Kata hiyo Bulambo ambayo ipo katika Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kajenge kwamba, utekelezaji tayari tumeanza kwa kuingiza kwenye orodha ya vituo vya afya vya kimkakati na

tutahakikisha kwamba fedha inapelekwa kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene.

Na. 535

**Upungufu wa Watumishi wa Afya Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la upungufu wa Watumishi wa Kada ya Afya – Bukene?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira kila mwaka, ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 jumla ya watumishi wa kada ya afya 34,720 wameajiriwa na kupangiwa vituo kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepangiwa jumla ya watumishi 111, ambao wamepangwa katika Hospitali ya Wilaya, vituo vya afya na zahanati. Kati ya hao, Jimbo la Bukene limepelekewa jumla ya watumishi 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa sekta ya afya kwa awamu na kuwapanga katika maeneo yenye upungufu wa wataalam hao ikiwemo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa Serikali kutupatia watumishi wa kada ya afya 59 kwenye Jimbo la Bukene, lakini nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati mpya tulizojenga na ambazo zimeanza kutoa huduma za vijiji vya Gulyambi, Buhulyu, Mogwa, Iboja, Ilagaja, Kasanga na Mboga, zote hizi zina mtumishi mmoja mmoja tu. Nyingine zina Mganga peke yake, hazina *nurse*, nyingine zina *nurse* peke yake hazina Mganga, kiasi ambacho huyu mtumishi mmoja akipata dharura tu zahanati inafungwa, kunakuwa hakuna huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kila zahanati mpya hasa hizi zinazoanza iwe angalau na watumishi wasiopungua wawili, mganga na *nurse* ili angalau hata mmoja akipata dharura kituo kisifungwe kabisa? Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hiyo *minimum* ya watumishi inakuwepo kwenye kila kituo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na kutekeleza kipaumbele chake na sera yake ya kusogeza huduma ya afya karibu zaidi na wananchi kwa kujenga zahanati ili kupunguza umbali wa wananchi kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka hii minne ya Serikali ya Awamu ya Sita jumla ya zahanazti zaidi ya 1,300 mpya zimejengwa zikiwemo zahanati ambazo zipo katika Jimbo la Bukene. Maana yake ni kwamba, tumeendelea kuongeza sana idadi ya vituo vya afya na *automatically* idadi ya watumishi wanaohitajika pia imeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bukene, Mheshimiwa Selemani Zedi kwamba tunafahamu katika zahanati hizo kuna upungufu wa watumishi, lakini kwa sababu zahanati hizo ni mpya,

tumeendelea kuajiri watumishi na kuwapeleka kwa ajili ya kuziba pengo la watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora kwamba, katika maeneo yote ambayo yana watumishi mmoja katika zahanati, wafanye msawazo wa ndani wa watumishi, iwe kutoka Halmashauri nyingine yenye nafuu kupeleka hapo pia ndani ya Halmashauri yenyewe kutoka kwenye vituo vingine vyenye watumishi wengi ili angalau huduma muhimu ziendelee kutolewa wakati Serikali inaendelea kutoa vibali vya ajira ili kwenda kuziba mapengo hayo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe nimekuona, atafuatia Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Serikali imetujengea vituo vipya vya kutoa huduma za afya (zahanati na vituo vya afya) pamoja na ukarabati wa hospitali ya wilaya, lakini tuna changamoto kubwa ya watumishi kwenye eneo hili la afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea watumishi wa afya kwenye maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba katika kipindi hiki cha miaka minne wataalamu wa Sekta ya Afya walioajiriwa ni wengi sana (wataalmu 34,720) lakini wataalamu hawa bado hawatoshi kwa sababu pia kasi ya ujenzi wa vituo imekuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inakwenda na utekelezaji wa afua zote za ujenzi wa vituo vya afya angalau visogee karibu na wananchi, lakini pia afua za kupeleka watumishi wa Sekta ya Afya kwa awamu ili kuhakikisha sasa ikama ya watumishi katika vituo hivyo inatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mafuwe, katika Jimbo la Hai tunafahamu vipo hivyo vituo vya afya ambavyo vimejengwa vipya, vimeongezeka lakini na Serikali inaendelea kupeleka wataalamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanatimiza majukumu yao ipasavyo na wananchi wapate huduma bora zaidi za afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Katika Mkoa wa Mtwara tumekuwa na tatizo kubwa sana la watumishi wa kada ya afya, lakini pamoja na mambo mengine ni tatizo la kuwahamisha watumishi bila kuwaleta wengine. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wale ambao wanawaleta wanabaki kutuhudumia sisi watu wa Mtwara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara ni miongoni wa mikoa 10 ambayo Serikali tumeainisha kwamba ina changamoto kubwa zaidi ya upungufu wa watumishi wa kada ya afya, elimu, na pia watumishi wa kada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila kibali cha ajira, watumishi wengi zaidi wanapangiwa kwa kipaumbele kwenye mikoa hii 10 yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wa Sekta ya Afya. Kwa hiyo, kwanza ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Tunza Malapo kwamba kila kibali cha ajira kitakapojitokeza tutahakikisha watumishi wengi zaidi wanapelekwa kwenye Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kumekuwa kuna wimbi la baadhi ya watumishi kuhamishwa kutoka kwenye halmashauri za vijijini au baadhi ya mikoa hasa hiyo 10 na kukimbilia maeneo ya mjini. Tumeweka utaratibu kwanza watumishi wanaohama

lazima wapate kibali cha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kujiridhisha sababu za uhamisho na hasa sababu zile za ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tumewaelekeza Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanajiridhisha pale watumishi wanapokuja na barua za uhamisho wajiridhishe kwamba barua hizo zimepitishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI lakini pia wajiridhishe kama wameshatimiza ile miaka mitatu angalau baada ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, lazima kuwe na maelekezo maalum kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kudhibiti wimbi la watumishi kuhama maeneo ya pembezoni kwenda katika maeneo ya mijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange ninakushukuru sana kwa majibu haya kwa Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge Mbunge wa Kilwa litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ndulane.

Na. 536

**Ujenzi wa Ukuta Pwani ya Mji wa Kilwa Kivinje**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE K.n.y. MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga ukuta eneo la Pwani ya Mji wa Kilwa Kivinje ili kuzuia maji ya Bahari yanayoathiri Wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi zinazochangia kuongezeka kwa kina cha Bahari na kuathiri fukwe mbalimbali ikiwemo eneo la Pwani ya Mji wa Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizo ni pamoja na kuendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa fukwe zote katika Ukanda wa Pwani ikiwemo Kilwa Kivinje na kuendelea kutenga fedha na kutafuta fedha kupitia Mifuko ya Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo, Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(Adaptation Fund), GEF* na *GCF* na Washirika wa Maendeleo ikiwemo Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, shughuli za ujenzi wa ukuta eneo la Pwani ya Mji wa Kilwa Kivinje zitaanza kutekelezwa baada ya fedha kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kuhimiza uongozi na wananchi wa Kilwa Kivinje kuendelea kuongeza jitihada za kutunza na kuhifadhi mazingira ya maeneo ya ufukwe na kudhibiti shughuli zisizo endelevu za kibinadamu na kuongeza jitihada za uhifadhi wa mazingira, upandaji wa miti kama ilivyobainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa kutujibu vizuri swali letu wananchi wa Wilaya ya Kilwa, lakini ningependa kuiomba Serikali iharakishe mchakato huo kutokana na umuhimu wa zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza kwamba ni lini Mheshimiwa Waziri atafika Kilwa ili kuweza kushuhudia hali halisi ilivyo katika Mji wa Kivinje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa kwa niaba, lakini nimwambie tu kwamba kwanza tumeshaanza mchakato wa uandikaji wa miradi kwa ajili ya kuomba fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchakato huu *the way* tutakapozipata fedha ndivyo ambavyo tutafanya haraka katika kuja kuanza angalau ujenzi; na kwa sababu tayari tumeshaanza tathmini ya awali, maana yake nimwombe tu Mheshimiwa kwa niaba ya wananchi wa Kilwa aendelee kuwa na Subira, mchakato huu umeshaanza na tutajitahidi tuharakishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kwenda Kilwa nimwambie tu kwamba Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo tayari na inafikia wananchi wote wa Tanzania ili kuona namna ambavyo tunatatua changamoto zinazowakabili wananchi zikiwemo hizi changamoto za maji ya bahari kuingia katika maeneo ya makazi na vipando visivyo stahimili maji ya chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu kwamba tupo tayari kwenda Kilwa kuona hali ilivyo na kuona namna ambavyo tunaweza tukawashauri na kuwasaidia wananchi, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya, nimekuona.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya maji kutoka kwenye bahari na kuingia kwa wananchi kupelekea madhara mengi ambayo Mheshimiwa Waziri ameya-*mention;* ukuta wa Sepwese, Pemba umejengwa takribani sasa hivi ni mwaka wa tatu na wananchi bado wanaendelea kupata changamoto hizi. Tunataka kujua kauli ya Serikali, mradi huu utakamilika lini kwa upande wa Sepwese, Pemba ili kunusuru madhara kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Asya kwani amekuwa mdau mzuri sana wa mazingira Zanzibar na maeneo mengine. Ninaomba nimwambie tu kwamba mara ya mwisho tulikwenda kwenye mradi wa Sepwese na kwa kweli tukakuta changamoto ya ule mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimwambie tu Mheshimiwa Asya kwamba hivi tunavyoongea, tayari mradi wa Sepwese wa ujenzi wa lile tuta umeshafikia 99% kwa maana kwamba ule mradi umeshakamilika. Kilichokuwa kinasubiriwa, ilikuwa ni sisi viongozi kama Wizara (Serikali) kwenda sasa kuwaambia wananchi na kuwakabidhi ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukwambie, kabla hatujamaliza Bunge hili tutakwenda Sepwese tukakabidhi mradi ili sasa, wananchi waendelee kutumia na wanufaike na ule mradi ambao umejengwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai na Mheshimiwa Asha nimewaona.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kwa mara nimekuwa nikisimama Bungeni hapa kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya umuhimu wa ujenzi wa ukuta katika maeneo ya fukwe za bahari kule Nungwi. Je, nilichokuwa ninataka kufahamu, ujenzi ule umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna maeneo mengi yamekuwa na changamoto hii ya maji ya bahari kutoka katika kina na kuingia kwenye makazi na kuingia kwenye vipando kama nilivyosema ambavyo havistahimili maji ya bahari. Changamoto hii ipo maeneo mengi; moja, ilikuwepo Sepwese

ambayo tayari tumeshaikamilisha; ipo pia Gando, Mikindani, Lindi na maeneo mengine ambayo yanaingia maji ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Simai kwamba kwanza ahadi hii tunaikumbuka na ndiyo maana kama atakumbuka katika bajeti ambayo tumeisoma hapa ya mwaka huu ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira katika zile shilingi bilioni 89 ambazo tumeidhinishiwa na Bunge hili tumesema moja miongoni mwa kazi tunayokwenda kuifanya ni kwenda kutatua changamoto ya uingiaji wa maji ya bahari sambamba na kujenga kuta za aina zote zinazohusika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa, fedha zile zitakapokuwa tayari, tutakwenda kujenga maeneo mengi lakini Nungwi tutakwenda kuipa kipaumbele. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma na Mheshimiwa Abdul nimewaona.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Tumepata maelezo mazuri jinsi Serikali itakavyoshughulikia maji kuongezeka katika fukwe za Bahari, lakini hali hii ya kujaa maji ipo pia katika maziwa yetu ambayo kuna sehemu nyingine miji pia imezama kabisa. Je, Serikali imejipanga vipi kufanya mkakati wa utafiti kwa jinsi itavyodhibiti maji yanavyojaa kwenye maziwa yetu na namna gani tuta-*save* maji haya kufanyia kazi nyingine badala ya kuzamisha miji yetu iliyopo katika maziwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali la mwazo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mara nyingi watu wamekuwa wakilia na kilio cha maji ya bahari kuingia katika makazi lakini ni kweli utafiti umeonyesha kwamba hata maji ya baadhi ya maziwa na mito mingine kina chake kinakuwa kikubwa na yanaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu jibu lipo pale pale kama tulivyoeleza katika jibu la msingi kwamba tumeanza kufanya utafiti kwa sababu hatuwezi kujenga ukuta kabla ya kufanya utafiti kujua aina gani ya ukuta unaotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaendelea kutafuta fedha na zitakapopatikana, nimwambie Mheshimiwa Asha na Waheshimiwa wote kwamba tunakwenda kujenga kuta kwenye maeneo yote yenye changamoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya mazingira hasa kwa maeneo ya bahari ambayo yanatumiwa na masuala ya Uchumi wa Bluu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo yameathirika kutokana na shughuli za Uchumi wa Bluu ambazo zinaendelea. Kama unavyofahamu kwamba Uchumi wa Bluu ni uvuvi, lakini vilevile masuala ya ulimaji wa mwani, masuala ya harakati za utafiti kwa ajili ya ugunduzi wa mafuta na gesi na mambo kama hayo. Kwa hiyo, shughuli hizi zimekuwa zikiharibu mazingira kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua hatua mbalimbali zikiwemo za kuendelea kutoa elimu kwa wananchi, kwanza namna ya kufanya shughuli za uvuvi ambazo zinazingatia sheria. Pia, tumekuwa tukiwaambia wananchi kwamba sababu nyingine inayoathiri ni sababu kubwa ya watu kukata mikoko ama miti iliyo pembezoni mwa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumeendelea kuwaelimisha wananchi kuwaambia kwamba pamoja na shughuli hizi zinazoendelea za Uchumi wa Bluu za uvuvi na mambo mengine, lakini miti iendelee kupandwa kwa sababu miti ndiyo uhai wa

bahari. Kikubwa tumehimiza watu masuala ya usafishaji wa fukwe na mambo mengine kama hayo ili shughuli za Uchumi wa Bluu ziendelee pia usafi, na sheria ya mazingira vizingatiwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira (Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis) kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 537

**Muswada wa Sheria Kuhusu Ndoa za Jinsia Moja**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta marekebisho ya Sheria ya Ndoa kuhusu ndoa ya jinsia moja au Muswada wa Sheria kupiga marufuku ndoa ya jinsia moja?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, ndoa imetafsiriwa kuwa makubaliano ya hiari kati ya mwanamke na mwanaume kuishi pamoja na inaweza kuwa ya mume mmoja na mke mmoja au mume mmoja na wake zaidi ya mmoja. Hivyo, sheria yetu haitambui ndoa ya aina nyingine yoyote isipokuwa kama ilivyotafsiriwa katika sheria tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ambapo tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Haki Jinai *(The Criminal Justice (Miscellaneous*

*Amendment) Bill)* ambapo Kifungu cha 176 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kimependekezwa kufanyiwa marekebisho ili kudhibiti vitendo vya ukiukwaji wa maadili ikiwemo vitendo vya ndoa za jinsia moja, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kumekuwa na ongezeko kubwa la ndoa za utotoni na kumekuwa na unyanyasaji wa hawa watoto ambao wanaolewa wakiwa wadogo. Serikali mna mkakati gani wa kukomesha ndoa za utotoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na manyanyaso sana ya wanawake kupigwa na kunyanyaswa wakiwa kwenye ndoa. Je, mmefanya utafiti wa kutosha kuona hayo manyanyaso yapo makubwa kiasi gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ndoa za utotoni kukomeshwa, ni kweli matukio haya yapo katika baadhi ya maeneo, lakini yanadhibitiwa kwa sheria mbalimbali ikiwepo Sheria ya Mtoto inayozuia mtoto kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji, unyanyasaji ikiwa ni pamoja na ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna imani sheria hiyo ikisimamiwa vyema ikiwa ni pamoja na wananchi kuielewa na kuchukua hatua za kutoa taarifa kwenye vyombo vya usimamizi wa sheria ili hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani, *then* tutakuwa tumesaidia kukomesha jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu kuliko yote ni wananchi wa Tanzania kuzingatia maadili, mila, na desturi zetu ambazo zinazuia mtoto kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji ili hatimaye tuwe na kizazi ambacho kipo katika malezi yaliyo bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu manyanyaso ya wanawake kupigwa ni jambo ambalo limepigiwa kelele mara nyingi na sheria zetu za jinai haziruhusu, na siyo mwanamke tu, bali hata mtu yeyote kupigwa. Kwa hiyo, inapotokea mwanamke kapigwa kwa sababu tu ya kuwa katika ndoa, sheria zinaruhusu mwanamama huyu kulalamika katika vyombo vya usimamizi wa sheria ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wanaume wanaokiuka misingi bora ya ndoa zetu ikiwa ni pamoja na kuepuka kuwapiga wake zetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt...

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Thea Ntara.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, endelea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, lakini umesahau jina langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni yale yaliyokusanywa na tukapewa muda kama mwaka mzima (mwaka jana), ni lini sasa mtaleta ile Sheria ya Ndoa hapa Bungeni? Ule Muswada mtauleta lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu la msingi la swali husika nimesema Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha kuandaa Muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali za Haki Jinai na swali kama anavyouliza Mheshimiwa Mbunge, (Dkt. Thea Ntara) litazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninakushukuru, ingekuwa kama utaratibu unaruhusu na mimi ningeuliza swali, lakini ahsante

nashukuru kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini aulize swali lake.

Na. 538

**Ujenzi wa Chuo cha VETA – Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilaya ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Kilwa ni miongoni mwa Vyuo 64 vya *VETA* vinavyojengwa na Serikali katika Wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi pamoja na Chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe ambao ulikuwa hauna Chuo cha *VETA* cha Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kilwa unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.6 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi 682,881,780.24 kimetumika. Aidha, ujenzi wa Chuo hiki umefikia 40% na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mkakati wa Serikali ulikuwa chuo hiki kingeweza kukamilika mapema na kuanza kudahili wanafunzi mwaka huu wa 2025, je, ni sababu zipi zilizopelekea zoezi hilo la ujenzi wa chuo hiki kuchelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ningependa kujua mikakati ambayo Serikali inayo katika kuhakikisha kwamba mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa katika vyuo vyetu vya *VETA* yanakwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia na sayansi hapa duniani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa chuo, kumetokana na changamoto ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa wakati. Hata hivyo, idadi ya sasa tayari Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa chuo na kwamba ujenzi unatarajiwa kukamilika kama nilivyojibu kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili juu ya namna ya kuandaa mafunzo yanayoendana na teknolojia ya sasa; katika kuhakikisha mafunzo yanatolewa na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi yanayoendana na maendeleo ya mabadiliko ya teknolojia, Serikali imefanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 23, pamoja na maboresho ya mitaala, ili kuhakikisha mafunzo yanazingatia maendeleo ya mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mitaala yote iliyoboreshwa na ambayo inatumika katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi imeweka mazingira ya kuhakikisha maendeleo ya mabadiliko na teknolojia yanapewa nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar, nimekuona.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Serikali ilishaamua kutujengea Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)*, Wilaya ya Nyang'wale, leo ni zaidi ya miaka minne chuo hicho hakijakamilika. Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa chuo hicho cha *VETA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'wale kwa ufuatiliaji wake kuhusu ukamilishaji wa Chuo cha *VETA* cha Nyang'wale. Namwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya kupitisha bajeti yetu ya Wizara ya Elimu, Serikali inakwenda kukamilisha vyuo vyote ambavyo viko kwenye *progress* ya ujenzi na Nyang'wale ikiwemo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji Njombe tuliahidiwa kujengewa Chuo cha *VETA* na eneo lilitengwa, lakini hatupo katika mpango huo. Nini mpango wa Serikali kujenga vyuo vya *VETA* kwenye halmashauri za miji ambazo tayari zina uhitaji mkubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua ukweli kabisa kwamba, umuhimu wa *VETA* kwa nchi yetu ni mkubwa sana. Ndiyo maana Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, ameweza kutoa fedha nyingi za ujenzi wa vituo hivi vya *VETA* katika wilaya mbalimbali na kwa sasa tunakwenda kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwahidi Mheshimiwa Mwanyika kwamba, katika awamu inayofuata baada ya hii ya

kwanza, ambayo fedha zimetolewa kwenda kwenye *site,* na Njombe itakuwemo.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi. Kumbe, unaendelea hapo hapo, haya.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Leo Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu kwa Wizara mbili, hongera sana.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Felix pale, kwa niaba.

Na. 539

**Zoezi la Upimaji Ardhi, Halmashauri ya *Kasulu DC***

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha zoezi la upimaji wa ardhi katika Halmashauri ya Kasulu *DC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 50 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikishwa viwanja 500 kupitia Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi *(KKK)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia fedha hizo, zaidi ya vipande vya ardhi 1,200 vilitambuliwa, viwanja 866 vimepimwa na kuidhinishwa katika Mitaa ya Nyangwa, Makere na Kalimungoma. Zoezi la kumilikisha viwanja 866 vilivyoidhinishwa linaendelea kupitia mazoezi ya Kliniki za Ardhi, Ofisi za Halmashauri na Ofisi ya Ardhi, Mkoa wa Kigoma, ambapo jumla ya Hatimilki 47 zimeandaliwa na kati ya hizo, 37 zimekabidhiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na zoezi la utambuzi na upimaji ardhi, kazi ya kuhuisha mipaka baina ya Vijiji vya Kagerankanda na Uvinza vilivyopakana na Msitu wa Hifadhi wa Makere Kusini pamoja na Kitalu cha Uwindaji ilifanyika, na pia, ukaguzi na uidhinishaji wa upimaji wa vijiji hivyo viwili unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, eneo ambalo wananchi wa Kitongoji cha Katoto watahamishiwa kupisha eneo wanaloishi kwa sasa limetengwa, ikiwa ni utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro katika vijiji/mitaa 975. Kadhalika, zoezi la urasimishaji makazi katika mitaa mbalimbali linaendelea, ambapo jumla ya viwanja 4,813 vimepimwa na kuidhinishwa katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kumekuwepo na migogoro ya mipaka kati ya vijiji na vijiji, wilaya na wilaya, mikoa na mikoa na Serikali ipo. Lini migogoro hii itaisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Kavejuru kwa swali lake. Ni kweli kabisa migogoro ipo na tunaendelea kupambana kuipunguza, na siku moja itamalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya vijiji na vijiji, kupitia Tume yetu ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi, ukweli imeonesha matokeo mazuri sana, na kwa sasa tunaendelea. Watu wako uwandani kwenye baadhi ya vijiji katika wilaya nyingi hapa nchini, kwa ajili ya kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi, ambao tumeona ni suluhisho la migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro kati ya wilaya na wilaya na mkoa na Mkoa, ni migogoro ya kiutawala. Mjue nchi yetu siyo mpya katika upimaji wa maeneo, isipokuwa kumekuwa na mgongano tu wa maeneo haya mawili kati ya wilaya moja na nyingine, na mkoa mmoja na mwingine. Tumeendelea na utatuzi katika kuwaelimisha watu umuhimu wa kuheshimu mipaka ambayo tayari ilikwishawekwa siku nyingi sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima James Mdee, nilikuona.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kuna zoezi la upimaji na uuzaji wa viwanja linaloendeshwa na Shirika la Maendeleo Dar es Salaam *(DDC)* katika Halmashauri mbili za Ubungo na Kinondoni, zoezi ambalo lina ugomvi na mgogoro mkubwa sana. Waziri aliahidi mbele ya Bunge kwenda kutatua mgogoro kati ya tarehe 2 na 7 mwezi wa Sita, leo ni tarehe 9 Juni, Waziri hajaonekana. Naomba majibu ya Serikali, Waziri ataenda lini na/au tutaongozana naye lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa jibu na ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa maswali ambayo amekuwa akiyajibu hapa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge Halima Mdee kwamba, hali yangu ya kiafya haikuwa nzuri wiki yote iliyopita. Kwa hiyo, sikupata nafasi ya kuweza kwenda, lakini nitakaa naye tupange tuweze kwenda, kama nilivyoahidi na sikuahidi hapa tu ndani ya Bunge lako Tukufu, niliahidi vilevile nilipokutana na wale wazee walipokuja katika Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, nitafika katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, nilikuona.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuna mgogoro mkubwa kati ya Kijiji cha Chilunda na Kijiji cha Lipupu. Je, Wizara iko tayari kumwelekeza Kamishna wa Ardhi, Mkoa wa Mtwara, kwenda katika vijiji hivyo, ili kutoa suluhu ya mgogoro huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mhata nadhani baada ya kumaliza kujibu maswali haya, tukutane ili tuweze kuliangalia kwa ukaribu, lakini nikubaliane na wewe kumwelekeza Kamishna wa Mkoa aende mara moja kwenye eneo hili la mgogoro na baadaye tupate mrejesho wa pamoja wa chanzo cha mgogoro.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda pamoja na Mheshimiwa Deo Ndejembi, kwa majibu mazuri ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Oran Njeza.

Na. 540

**Hitaji la Makoti ya Baridi kwa Askari - Mbeya**

**MHE. ORAN M. NJEZA K.n.y. MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawapa makoti ya kujikinga na baridi Askari Polisi wanaofanya kazi katika Mkoa wa Mbeya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, makoti ya kujikinga na baridi ni miongoni mwa sare za Jeshi la Polisi, ambazo Askari wanaofanya kazi kwenye mikoa yenye hali ya hewa ya baridi kali hupatiwa. Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo Askari Polisi wanapewa makoti ya kujikinga na baridi kali wakiwa kazini, kama sare ya Jeshi la Polisi. Mikoa mingine inayopewa makoti ya kujikinga na baridi ni Iringa, Njombe, Songwe, Rukwa, Arusha, Manyara, Kilimanjaro pamoja na Wilaya ya Lushoto katika Mkoa wa Tanga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kutoa pole kwa wafiwa pamoja na majeruhi waliotokana na ajali mbaya iliyotokea Mlima Iwambi, Mbalizi, Mbeya. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awasaidie majeruhi wote waweze kupona kwa haraka na Marehemu wote azilaze roho zao mahali pema Peponi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Askari hawa mara nyingi wako kwenye doria na wengine wako kwenye sehemu za ukaguzi wa magari, je, ni lini Serikali itajenga vibanda vya ukaguzi katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mbalizi, wananchi pamoja na Serikali wamejenga Kituo cha Polisi cha Wilaya. Je, ni lini sasa Serikali itajenga nyumba za Askari wa Kituo hiki cha Wilaya ya Mbalizi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Askari wetu wanafanya kazi nzuri sana, kwa maana ya doria pamoja na ukaguzi na yapo baadhi ya maeneo tayari tumeshajenga mabanda hayo, kwa ajili ya Askari wetu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, maeneo aliyoyataja pia tutayaweka kwenye mpango kwa ajili ya kujenga mabanda

hayo, ili Askari wetu wanaofanya doria na ukaguzi, wapate maeneo ya kujisitiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la pili, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mbalizi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya ujenzi wa Kituo cha Polisi. Ninakumbuka pia, Serikali iliunga mkono juhudi za wananchi hao kwa kutoa shilingi milioni 100 ambayo tayari ilishafika ya ujenzi wa Kituo cha Polisi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaweka kwenye mpango sasa ujenzi wa nyumba za Askari wetu kwa ajili ya eneo la Mbalizi ambao wanafanya kazi nzuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Kata ni kati ya Askari ambao wanasaidia sana ulinzi wa raia na mali zao katika kata zetu, hasa zile ambazo ziko maeneo ya vijijini, lakini wamekuwa wakifanya kazi kwa mazingira magumu sana; hawana usafiri, wanawajibika kutumia fedha zao kuzunguka katika kuhakikisha kwamba, wanaimarisha ulinzi na usalama, zaidi wanawajibika kushiriki kwenye shughuli za kijamii kwa kutumia fedha zao za mfukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu sasa wa kuwatengea walau *package allowance* kidogo ya kuwawezesha kuzunguka kwenye shughuli za kijamii, ikiwemo kupeleka pikipiki kwa hao Polisi Kata kote nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Askari Kata wanafanya kazi nzuri sana kwa ushirikiano na jamii. Serikali kwa kutambua kazi kubwa wanayofanya tayari imeshasambaza pikipiki 105 kwa Askari Kata hapa nchini na bado mpango unaendelea kuhakikisha kwamba, kwanza tunajenga Ofisi za Polisi Kata kwenye kata zote pamoja na shehia kwa upande wa Zanzibar, lakini pia, tunawapatia vitendea kazi, kama pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema, tayari tumeshatoa pikipiki 105. Kwenye bajeti hii tumetenga fedha, kwa ajili ya kuhakikisha tunawapatia pikipiki ili kurahisisha utendaji kazi wa hao Askari Kata. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 541

**Elimu ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani - Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa Wakulima ili kuondoa changamoto zilizopo - Singida Kaskazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Selemani Jafo, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala *(WRRB)* na wadau wengine katika Mnyororo wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ilibaini uwepo wa changamoto ya uelewa kuhusu mfumo unavyofanya kazi kwenye baadhi ya maeneo, hivyo kusababisha kuundwa kwa timu maalum, ili kutoa elimu katika Mikoa ya Singida, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala imetolewa na itaendelea kutolewa katika ngazi ya Halmashauri na Kata zote nchini zinazozalisha mazao

mbalimbali, ikiwemo dengu na mbaazi katika Mkoa wa Singida, Jimbo la Singida Kaskazini katika Kata za Mwasauya na Msange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la utoaji wa elimu kuhusu matumizi ya mfumo huo itakuwa endelevu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na hayo majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Pamoja na juhudi hizo ambazo zimefanywa na Serikali, lakini kuna *AMCOS* ambazo hazikulipwa kwa hiyo, kumekuwa na kucheleweshwa kwa malipo ambayo kwa msimu uliopita wa 2024, mpaka sasa bado wananchi wanadai, ikiwemo *AMCOS* ya Ngamu pamoja na ya Ngimu. Sasa ni utaratibu upi uliopo kwa ajili ya kuhakikisha suala hili la kuchelewesha malipo linaondolewa, lakini pia, na hawa ambao hawajalipwa walipwe?

Mheshimiwa mwenyekiti, swali la pili. Kuna maghala mengi hayajasajiliwa, suala ambalo linawapa usumbufu mkubwa sana wananchi. Ni ghala moja tu la Mtingo limesajiliwa, lakini Maghala ya Mdeda, Makulo, Kinyeto, Ngimu, Mwasauya hayajasajiliwa, kwa hiyo, wananchi wanapata shida kuweza kwenda kupeleka mazao yao.

Mheshimiwa mwenyekiti, sasa ni utaratibu upi unafanyika kwa haraka kuweza kuyasajili maghala haya tunapoelekea kwenye msimu wa mwaka huu wa mauzo ya biashara, ikiwa ni pamoja na kuweka uwazi kwenye minada, kwa sababu, minada ile inafanywa kwenye mtandao na wananchi wengi wanatumia viswaswadu, ambavyo haviwezi kupata *access to information*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza ndugu yangu, Mheshimiwa Abeid, Mbunge, kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwanza naomba niweke rekodi vizuri. Katika kipindi kilichopita waliuza tani 16,900 ambapo hii ilikuwa ni dengu peke yake. Zaidi ya shilingi bilioni 30.5 zilienda kwa wananchi, kwa hiyo, hii ni faraja kubwa sana. Hivi karibuni, mpaka juzi, suala zima la ufuta tayari wameshakusanya karibu tani 1,800 ambazo zina gharama ya shilingi bilioni 4.4. Hizi zote ni fedha kwa upande wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande huu sasa *AMCOS* ambazo wananchi bado hawajalipwa, ngoja tulifanyie kazi kwa sababu, katika rekodi zetu tulikuwa tunafanya *compliance* maeneo yote na ilionekana katika kipindi kilichopita, maeneo ya Kyela ndiyo yalikuwa na changamoto kidogo, hata hivyo, yalifanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala la Singida ngoja tulifanyie kazi tuone wapi changamoto ilijitokeza. Lengo ni kuhakikisha watu wanapata haki yao ya msingi. Naomba nimwagize Mtendaji Mkuu wa Maghala, Asengi Bangwa, afuatilie haraka na anipe mrejesho ili wananchi waweze kupata fursa yao ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa maghala ambayo hayajasajiliwa, Taasisi yetu ya Bodi ya Stakabadhi Ghalani inafanya hii kazi na sasa hivi tumesajili maghala mengi. Maghala ambayo tumeyasajili mengine sasa hivi tumeyawekea *CCTV Camera* kwa lengo la ku-*track information* zote katika *real time data*.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa upande wa Singida, namwagiza tena Mkurugenzi, Bwana Bangwa, afuatilie kwa haraka kuhakikisha maghala yote ambayo hayajasajiliwa yanaingizwa katika mfumo. Lengo letu kubwa ni wananchi waweze kuuza mazao yao kupitia mfumo huo ambao una faida kubwa sana katika nchi yetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia maghala yanayomilikiwa na watu binafsi kununua mazao ya wakulima, hasa kwa maeneo ambayo haina maghala, ili kuongeza ushindani kwa wakulima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hili swali la Mheshimiwa Mbunge, ambaye ni mtaalamu mzuri sana wa kilimo, kutoka pale *SUA*. Suala la usajili wa maghala binafsi tumeshalifanyia kazi, hata na Kamati ya Bunge, ninakumbuka tulivyoenda Shinyanga pale kwa sababu, siyo maghala yote, ni ya Serikali, sasa hivi mengi yametengezwa na *private sectors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba watu binafsi, kwanza waendeleze juhudi hii ya utengenezaji wa maghala kwa sababu ni biashara, lakini hata hivyo, Serikali imefungua milango maghala haya yasajiliwe kwa lengo la kuhakikisha kwamba, bidhaa hizo zinaingizwa katika maghala haya na biashara ifanyike. Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili linafanyika hivi sasa na maghala haya mengi kutoka katika sekta binafsi yanasajiliwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, nilikuona.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni suala la *account* za wakulima kulala ndani ya miezi sita bila ku-*operate*. Je, kwa mazingira ya wakulima, Serikali haioni umuhimu wa kuondoa sheria hii kuifanya *account* ya mkulima iweze ku-*operate* bila kulala?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mpakate. Miongoni mwa mikoa ambayo inafanya vizuri ni Mkoa

wa Ruvuma ambao uko katika jimbo la ndugu yangu Mheshimiwa Mpakate. Kwenye hili Serikali ni lazima tu-*appreciate* kazi kubwa na inayoendelea vizuri. Niwaombe wananchi wa kule wamwone vizuri ndugu yangu Mheshimiwa Mpakate kwa kazi hii kubwa anayoendelea kuifanya, na hasa kipindi hiki cha lala salama kuamkia gazetini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *account* tunalifanyia kazi. Lengo letu ni kwamba tuone kama kuna changamoto yoyote ya kifedha. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba kila mwananchi *accoun*t yake inafanya kazi. Hili Mheshimiwa Mpakate tuonane baadaye ili tuelezane vizuri changamoto iko wapi, tuboreshe vizuri ili wananchi wetu wapate fursa ya kufanya biashara yao katika mazingira mazuri, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Selemani Jafo kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Wizara ya kilimo, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, aulize swali lake.

Na. 542

**Kupitia Upya Mikataba ya Mashamba ya Ushirika**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni ipo haja ya kupitia upya mikataba ya mashamba ya ushirika na kufanya tathmini ya ardhi ya mashamba hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika inafanya mapitio na tathmini ya mikataba ya uwekezaji katika mashamba ya ushirika. Baadhi ya mikataba inayoendelea kufanyiwa mapitio ni ya mashamba ya Vyama vya Ushirika vya Miradi ya pamoja ya

Kyumasha, Murososangi, Fonrwa, Lyamungo Amcos, Manush Narumu; Mashamba ya Vyama vya Ushirika vya Kilimaboro, Masama Mula, Kibosho Kati na Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeweka moduli ya uwekezaji kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) kwa lengo la kufanyiwa upembuzi na tathmini. Hadi sasa jumla ya mashamba 408 ya vyama vya ushirika yenye thamani ya shilingi bilioni 271.48 yameingizwa kwenye mfumo huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inaendelea kufanya tathmini kwenye mashamba haya, na kwa kuwa wananchi hawajashirikishwa, na kwa kuwa migogoro inaendelea kujitokeza kati ya wawekezaji na vyama vya msingi pamoja na wananchi, je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kusitisha kwanza kwa muda mkataba wa Chama cha Ushirika cha Fond; kwa maana ya *For Nronga Warry* ili kwanza tathmini hiyo ifanyike na mkataba uwe shirikishi ndipo mkataba huu uweze kusainiwa na kuepusha migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa kumekuwa na migogoro mingi inayotokana na kutokushirikishwa kwa wadau wengi wanaohusika na ushirika na kuzalisha migogoro isiyokuwa na sababu, je, Serikali haioni kuwa ipo haja kwa mikataba hii kuhusishwa kwenye Wizara ya Mipango na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili mikataba hii ipitiwe vizuri ili ikisainiwa iwe na tija kwa Serikali na kwa vyama vya ushirika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nimpongeze sana Mbunge wa Jimbo la Hai Mheshimiwa Mafuwe hususan kwa kupigania vyama vya ushirika katika jimbo lake kwa muda wote wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu kwamba, moja ni kwamba tutaendelea kufanya tathmini, na nimeshawaelekeza Tume ya Ushirika, kwamba wasisaini mkataba wowote bila kuwashikirisha wananchi. Kwa hiyo, hata katika chama cha ushirika eneo la Fongo hicho cha Nronga Warry maelekezo ni hayo hayo, kwamba, wawashirikishe wananchi, wananchi waridhie ndipo mkataba huo uweze kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na haja ya Serikali kushirikiana na Wizara ya Mipango na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ni sehemu ya maelekezo ambayo tumeshapatiwa sasa hivi kuanza kuyapitia. Kwa hiyo, jambo hilo lipo katika mipango ya Serikali na tutaanza kulitumia katika mikataba yote inayofuata baada ya sasa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa David Ernest Silinde kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Kilimo. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale litaulizwa na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 543

**Huduma ya Bure ya Mtandao Vyuoni na Shuleni Nchini**

**MHE FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka huduma ya bure ya mtandao kwenye vyuo na shule zote nchini?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UCSAF* imefanikiwa kufikisha *internet* katika maeneo sita ya umma kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba (Mafinga), eneo la Bustani ya Nyerere *Square* (Dodoma), Ndaki ya Habari na Elimu Angavu (Chuo Kikuu cha Dodoma), Soko la Tabora, Kiembe Samaki (Unguja) na Soko la Buhongwa (Mwanza) na maeneo mengine 17 katika viwanja vya maonyesho ya Saba Saba. Lengo la Mradi huu ni kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya *internet* ya kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *UCSAF* imekuwa ikitekeleza mradi wa kuzipatia shule za Serikali vifaa vya TEHAMA ili kuziunganisha na mtandao wa *internet*, ambapo mpaka sasa takribani shule 1121 zimenufaika kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hii ya kufikisha huduma ya *internet* katika maeneo ya vyuo na katika shule za Serikali unaendelea kadiri ya upatikanaji wa fedha kwa lengo ya kuzifikia shule zote na maeneo yote yenye uhitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa jitihada hizi kubwa ambazo inazifanya za kuhakikisha kwamba inasogeza huduma ya *internet* kwenye maeneo yetu ya vyuo na kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Kuchauka ana swali lake la kwanza, anasema; kwenye Jimbo la Liwale shule nyingi hazina *access* ya *internet* na maeneo mengi hayana kwa sababu mitandao mingi iliyofungwa pale inatumia *solar*. Kwa hiyo, nyakati za usiku na nyakati za jioni ambapo umeme umepungua kunakuwa na kukosekana kwa mawasiliano. Je, ni lini Serikali itahakikisha imefikisha umeme kwenye maeneo hayo ili *internet* iweze kupatikana kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Makete ambalo mimi ndio Mbunge wao. Tunaomba kuuliza, ni lini minara ambayo haijakamilika ya *UCSAF* ambayo tulipatiwa kwa mfano Usalimu *One* na kule Ruhumbu, ni lini minara hii itakuwa imekamilika kujengwa ili wananchi wa maeneo haya waweze kupata *internet* ya kutosheleza na waweze kufurahia maisha ya Taifa lao?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Festo Sanga kwa uwajibikaji wake na namna ambavyo ameweza kumwakilisha Mheshimiwa Kuchauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Liwale mitandao mingi inatumia *power* ya *solar* na wakati mwingine, hasa wa jioni wanapotea, lakini tumshukuru sana Mheshimiwa Rais tayari *REA* ina inaendelea kusogeza huduma ya umeme maeneo hayo yote ambayo umeme wa uhakika wa *Grid* ya Taifa haujawafikia. Kwa hiyo, niwaondoe hofu, muda siyo mrefu ninaamini na wao watapelekewa umeme wa *REA* katika maeneo yote haya pamoja na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake kwamba ni lini minara itakamilika katika jimbo lake Mheshimiwa Festo Sanga; kazi zinaendelea. Kadiri tunavyopata fedha tutaendelea kuhakikisha kwamba minara hii ambayo tuliiweka katika maeneo ambayo walikubaliana inatakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata kwenye maeneo mengine ambayo hayajapatiwa bado uelekezi wa ujenzi wa minara, nimtoe hofu, kote tutafikia. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapatiwa huduma ya mawasiliano ya uhakika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba suala la mitandao kwa maana ya *internet* ya bure katika vyuo vyetu ni jambo muhimu sana. Hivi haoni kwamba ni muhimu sana kwa Serikali kuja na *program and plan of actions* (mpango kazi) kuonyesha mkoa gani utaweza kufanyiwa lini, ili watu wakajitayarisha na kuweza kupata manufaa ya kupata *internet* ya bure katika vyuo vyetu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali kutoka kwa Mheshimiwa Abbas Tarimba. Mpango kazi upo. Ukinisikiliza katika jibu langu la msingi nimesema nje na haya ambayo yameshafanyiwa, lakini tuna maeneo mengine 17 ambayo *UCSAF* imesha-*spot* kwenda kufanya. Kwa hiyo kuonyesha lini, wapi kitafanyika, niwe nimepokea. Waheshimiwa Wabunge, wataletewa mpango kazi huo ili kila mmoja aweze kufahamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani nilikuona.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini minara ya Kata ya Litehu, Ngunja na Michenjele itajengwa, kwa sababu mwanzo Waziri aliyekuwa mwenye dhamana aliahidi kupeleka minara maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Katani, lini minara itajengwa? Ahadi ya Serikali ni lazima itekelezwe. Kama Mheshimiwa aliyepita aliagiza, maana yake wataalam wana taarifa hizi. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge mwaka ujao wa fedha tutahakikisha kwamba tunaanza ujenzi katika maeneo hayo aliyoyataja.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi kwa majibu hayo ya Waheshimiwa

Wabunge kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Dorothy Kilave.

Na. 544

**Ujenzi wa Barabara ya Makondeko – Kwembe – Mloganzila**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, lini Serikai itakamilisha ujenzi wa barabara kutokea Makondeko – Kwembe hadi Mloganzila?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANROADS* imekuwa ikijenga barabara ya Makondeko – Kwembe – Mloganzila yenye urefu wa kilometa 17.26 kwa awamu, ambapo kilometa 4.89 zimejengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mloganzila – Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia *TANROADS* imepanga kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa urefu wa kilometa 1.7. Kwa sasa mradi upo kwenye hatua za manunuzi ya kumpata mkandarasi atakayetekeleza kazi za ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini ukiangalia sana, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inakwenda mpaka Mloganzila kwenye kituo cha afya. Je, hawaoni kwamba iko haja ya kumaliza haraka hizi kilomita 1.7 zilizobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, *TANROADS* hawaoni kwamba sasa iko haja kubwa ya kuanza barabara ambayo inaanzia Sudan Jimboni Temeke mwisho kuelekea kwenda Soko Kuu la Tandika mkabala na *Police Post* ya Tandika, kwa sababu barabara hii ni muhimu sana kwa kuwa inapitisha magari makubwa ambayo sidhani kama *TARUR*A wana uwezo nayo; ili magari yale makubwa yanapopita yanapoleta bidhaa kutoka mikoani iwe sahihi kwa sababu sasa hivi imebomoka sana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua hii barabara ilivyo na umuhimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba leo nimepata taarifa kuwa mkandarasi tayari ameshapatikana kukamilisha hizo kilomita 1.7. Pia barabara hiyo tumeitengea fedha kwa mwaka ujao wa fedha. Hii ninayosema ni kwa mwaka huu, lakini pia imetengewa fedha katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii Barabara ya Sudan – Soko Kuu la Tandika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi pamoja na wenzetu wa *TARURA* tutasaidiana kuhakikisha kwamba tunaupa umuhimu wa aina yake ili kwanza iweze kukarabatiwa, lakini pia kuijenga vizuri kulingana na hadhi na eneo lenyewe na magari yenyewe yanayopita hapo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tadayo nimekuona.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itakamilisha kwa kiwango cha lami barabara ya Mwanga – Kikweni – Kifula – Vuchamangofi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ikijengwa kwa awamu na tuko hatua za mwisho. Mkandarasi yuko ambaye anaendelea kilomita hizo tatu, lakini bado kilomita tano ambazo zimepangwa kujengwa katika

mwaka wa fedha ujao. Hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo kwa mwaka ujao kutoka Kikweni hadi Vuchamangofi itakuwa imekamilika kwa hizo kilomita tano ambazo zimebaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Mariam nimewaona.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Barabara ya Mabogini – Kahe iko chini ya *TARURA,* lakini ilishaombewa kuja *TANROADS* ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ikishapandishwa hadhi, ikishakuja kwetu, ndiyo tunapangiwa bajeti; lakini kama tutakuwa tumechukua maana yake bajeti ambayo ilikuwa imepangiwa *TARURA* tutaendelea kutekeleza kwa bajeti hiyo hiyo ya *TARURA*. Kwa upande wa *TANROADS* wakati sasa itakapokuwa tunaipangia bajeti, tutaipanga kwa utaratibu wa *TANROADS* na kama inatakiwa ifanyiwe usanifu upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba changamoto ambayo tumekuwa tunaipata wakati mwingine ni pale ambapo hadhi ya barabara za *TARURA* zinakuwa na upana wa mita 30, lakini zinapokuja *TANROADS* tunatakiwa tuongeze. Hapo ndipo panapokuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza tukaichukua moja kwa moja ama tukakasimiwa kuendelea kuifanyia matengenezo lakini ikiwa kwenye vipimo vilevile vya *TARURA* wakati tunaandaa fedha ya kulipa hizo mita 60, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam nilikutaja, Mheshimiwa Butondo na Mheshimiwa Anatropia watamalizia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuziba mashimo katika eneo la Vetenari Makutano na Barabara ya Mandela ambapo hali ya eneo hilo ni mbaya sana, na kwamba magari yanashindwa kupita?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara kubwa katika Mji wa Dar es Salaam. Nitoe maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Dar es salaam aende akafanye tathmini, na hiyo kazi ya kuziba hayo mashimo iweze kufanyika kwa uharaka unaowezekana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Barabara ya Kolandoto kwenda Munze hadi Mwangongo kilomita 63 katika kiwango cha lami, waliahidi kuwa watatekeleza mwaka wa fedha uliopita. Je, ni lini sasa utekelezaji wa mradi huu utaanza kufanyika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipanga kutekeleza hiyo Barabara ya Kolandoto – Mwangongo, na ndiyo barabara inayoenda Lalagwa hadi Sibiti. Tutaanza kujenga na tulishasaini mkataba Lalago kwenda Nkamo, lakini kwa upande wa Mwangongo hadi Kolandoto tumeendelea kuitengea fedha hata mwaka ujao wa fedha ili tuweze kujenga kipande hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Kyerwa ni moja kati ya wilaya ambayo haina kilomita hata moja ya lami. Sasa ninataka kujua, je, ni lini

Barabara zetu za Omugakorongo kwenda Murongo pamoja na Bugene kwenda Kaisho zitaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara tatu ambazo ziko kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami katika Wilaya ya Kyerwa. Kwanza ni Omurushaka kwenda Nkwenda ambapo mkandarasi tulishampata, Omugakorongo kwenda Murongo tayari iko kwenye manunuzi, pia Bugene – Burigi – Chato kwenda Kasumo mkandarasi yuko *site* akiwa anafanya kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mbunge wa Nyang'hwale.

Na. 545

**Kutangaza Mshauri Elekezi Barabara ya Kahama – Busisi**

**MHE. HUSSEIN M. AMAR** aliuliza: -

Je, lini Mshauri Elekezi atatangazwa kuanza kazi ya Upembuzi Yakinifu barabara ya Kahama – Kharumwa – Nyang'hwale hadi Busisi ambayo ni ahadi ya muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imempata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga barabara ya Kahama – Kharumwa – Nyang'hwale hadi Busisi kwa kiwango cha lami. Taratibu za kusaini mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. HUSSEIN M. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kupokea ombi langu la kumtafuta mpembuzi yakinifu na kuianza kazi hiyo. Swali langu la kwanza, je, kazi hiyo itaanza lini na kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa tunakwenda kulifungua Daraja la Kitaifa na Kimataifa Busisi - Kigongo Feri kwa kutokea Mwanza kwenda Shinyanga mpaka Kahama na kutokea Kahama kwenda Mwanza kwa kupitia Nyang'hwale, tofauti yake ni kilomita 90; tunatarajia baada ya kufunguliwa daraja hilo kutakuwa na magari mengi sana ambayo yatapita Daraja la Kigongo kwenda Kahama kwa kupitia Nyang'hwale; Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha za matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nassor, Mbunge wa Nyang'hwale, kwa kufuatilia hii kazi na mara kadhaa ameulizia, lakini tumefika tamati. Ni suala la muda tu lini tuisaini hiyo barabara ili iweze kuanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na ni kuanzia Mkoa wa Geita - Nyang'hwale, Nyang'hwale - Busisi na Nyang'hwale kwenda Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ninataka nitumie nafasi hii kwamba ni kweli Daraja la Kigongo Busisi maarufu kama Daraja la John Pombe Magufuli (JPM) litafunguliwa rasmi tarehe 19. Tunategemea Mheshimiwa Rais mwenyewe atakuwepo kufungua mradi huu wa kielelezo. Nitumie nafasi hii kuwaalika wananchi wote wa Tanzania pamoja na Wabunge kwenda kushuhudia tukio hilo la kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sambamba na hilo tunatambua kwamba ni kweli kutoka Kahama kwenda Mwanza itakuwa ni karibu sana kupitia hiyo njia. Nimhakikishie Mheshimiwa Nassor, Mbunge wa Nyang'hwale, kwamba kama Wizara na

*TANROADS* tushawaelekeza kwamba wahakikishe kwanza wanaimarisha hiyo barabara kwa sababu tunajua itakuwa na magari makubwa yatakayobeba mizigo baadaye. Pengine yatapungua sana kwenda Kahama ili wakati tunafanya usanifu lakini tuwe na uwezo pia wa kupitisha magari makubwa katika hiyo njia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista, nimekuona.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi anayejenga Barabara ya *Kibosho Shine,* Kwa Rafael mpaka *International School* ambapo ameondoka *site* baada ya kudai pesa shilingi 1,700,000,000 kwa muda mrefu na hivyo barabara ile ime-*stack* na wananchi wanapata adha kubwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ilimweka huyo mkandarasi na tunavyoongea tumeshapokea hati zake za malipo na tumeshawasilisha kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha na wametuambia kipindi hiki cha mwezi huu Juni, *certificate* nyingi (hati za malipo) zitalipwa ikiwa ni pamoja na ya mkandarasi huyu wa *Kibosho Shine* ili aweze kurudi na kukamilisha kazi ambayo alishaianza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea sasa na swali letu la mwisho kwa siku ya leo kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Zaytun Swai.

Na. 546

**Ujenzi wa Barabara kutoka Wasso hadi Loliondo Kilometa 10**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Wasso hadi Loliondo kilomita 10 utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Wasso hadi Loliondo yenye urefu wa kilomita 10 ni sehemu ya Barabara ya kutoka Mto wa Mbu hadi Loliondo yenye urefu wa kilometa 217. Serikali tayari imeanza taratibu za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa kuanza na sehemu ya Wasso hadi Loliondo yenye urefu wa kilometa 10 ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 5 Juni, 2025 na taratibu za kuanza kazi za ujenzi zinaendelea. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wananchi wa Ngorongoro bado wanataka kufahamu ni lini Barabara ya kutoka Wasso hadi Loliondo ujenzi wa lami utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wananchi wa Wilaya ya Monduli wamesubiria kwa muda mrefu sana barabara ya kutoka Kigongoni - Selela hadi Engaruka ni barabara yenye urefu wa kilometa 26 kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Je, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lini itakamilika hii Barabara ya Wasso kwenda Loliondo, tumesema tumeshasaini na baada ya kusaini tunategemea mkandarasi aanze kazi. Tutakachohakikisha ni kwamba tunamsimamia huyo mkandarasi ili aweze kukamilisha kipande hicho kwa muda na kuhusu barabara aliyoitaja ni kwamba tuna vipande kadhaa

ambavyo tuna Mto wa Mbu hadi Selela, Selela hadi Engaruka na Engaruka hadi Ngare Sero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vipande vyote hivi viko kwenye utaratibu wa kuanza kuvijenga kwa kiwango cha lami na yalikuwa ni maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, lakini pia kama Serikali tumeipangia katika mwaka huu iweze kutangazwa na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Esther Matiko nimewaona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Rau - Shimbwe na Rau – Kinyamvuo kupitia Mamboleo ni ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa awamu tatu mfululizo. Leo tunataka kufahamu ni lini barabara hiyo itaanza kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ahadi za Viongozi na hasa wa Kitaifa huwa ni kipaumbele. Hivyo, nimhakikishie kwamba *TANROADS* pamoja na wenzetu wa *TARURA* tutahakikisha kwamba ahadi za hawa viongozi zinatekelezwa ili wananchi hawa waweze kupata huduma ya barabara za kiwango cha lami kama zilivyokuwa zimeelekezwa na Viongozi wetu wa Kitaifa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Utegi – Shirati mpaka Kirongwe ambayo inaunganisha upande wa Kenya ni barabara ya muda mrefu sana tangu Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Mkapa. Je, ni lini sasa Serikali itaweza kukamilisha kipande hiki cha lami ambacho ni muhimu sana kwa uchumi wa Mara? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunavyoongea hii barabara tulishaitangaza, kwa hiyo iko kwenye hatua za manunuzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Ngerengere – Mvuha kwenda Kisaki hadi Mtemele *Junction* ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa hii barabara tutafanya mapitio, lakini kwa maana ya Mvuha kuja Bigwa tulishasaini mkataba, tunasubiri malipo ya *advance* ya mkandarasi hizo kilometa 78. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha, nimekuona.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Moshi – Arusha tuliambiwa mkandarasi amesh aripoti, lakini mpaka sasa hivi hatumwoni *site* na alitakiwa awe ameanza kulipa fidia wananchi kupisha Daraja la Kikafu. Je, ni lini tutamwona kwa macho mkandarasi akiwa *site*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niseme kwamba hiyo barabara ambayo tunasaidiana na wenzetu wa *JICA* inafanyiwa mapitio upya pamoja na kupatikana kwa mkandarasi, lakini imelazimika kuwe na mapitio upya ya usanifu ili iendane na hizo njia nne ikiwa ni pamoja na hilo Daraja la Kikafu. Tunaamini muda si mrefu ujenzi wa barabara hii

utaanza ambapo ni kutoka Arusha – Kikafu pamoja na barabara za Mji wa Moshi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha barabara ya lami ambayo inakwenda kwenye Halmashauri yetu Naguruwe – Mkunwa na Hiyari – Mkunwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote za *TANROADS* mipango yake ni kuwa barabara za kiwango cha lami, lakini barabara zote haziwezi kujengwa kwa wakati mmoja ikiwa ni pamoja na hiyo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kadri Serikali itakavyokuwa inapata hela basi hiyo barabara tutaijenga na hasahasa kama inakwenda kwenye makao makuu ya halmashauri. Ni moja ya vipaumbele vya Serikali kuunganisha makao makuu ya mikoa na halmashauri ama makao makuu ya wilaya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, nimekuona.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuelezwa kwamba mkandarasi wa kujenga Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe ameshapatikana, lakini mpaka leo kuna ukimya. Mheshimiwa Waziri ni lini mkataba utasainiwa ili mkandarasi aende kazini akafanye kazi ya kuwajengea barabara watu wa Korogwe na wa Bumbuli? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, tunachosubiri kwa kweli ni malipo ya awali ya huyo mkandarasi ili aweze kusaini na kuanza kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika na maswali yetu kwa leo ni hayo. Sasa ni wakati wa kutangaza wageni waliopo Bungeni leo hii.

Kwanza, tuna wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tuna wageni wawili ambao ni Watumishi wa Idara ya Bajeti kutoka Bunge la Ghana: Dkt. William Kafui Assem, Mkurugenzi wa Bajeti; na Ndugu Agget Adjoa Kapouchieneh, Afisa Bajeti Msaidizi, karibuni sana. *You are most welcome to our Parliament in Tanzania*. *(Makofi)*

Tuna wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ambao ni wanafunzi aliosoma nao Chuo Kikuu cha *St. Agustine* cha Jijini Mwanza *(SAUT MBA - Class of 2013)*. Karibuni sana wanafunzi ambao mmesoma na Mheshimiwa wetu. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Ndugu Brighton Babile, Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Shule ya Feza *International* kutoka Salasala Jijini Dar es Salaam. Karibu sana mtoto wetu wa Mheshimiwa Esther Bulaya ambaye unakamilisha masomo yako ya kidato cha sita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge: wageni watatu wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni wapiga kura wake kutoka Babati Vijijini Mkoani Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ambao ni Madiwani kutoka Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, ambao ni wifi zake kutoka Mkoani Mtwara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, ambao ni Machifu kutoka mikoa mbalimbali nchini. Karibuni sana machifu wetu kutoka mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Tuna wageni 29 wa Mheshimiwa Venant Daudi Protas, ambao ni waandishi wa habari kutoka Mkoani Tabora. Karibuni sana waandishi wetu wa habari. *(Makofi)*

Tunao pia, wageni 49 wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, watumishi wa Idara ya Afya kutoka Halmashauri ya Mwanza Jiji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ambao ni wapigakura wake kutoka Hai Mkoani Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Mgeni wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ambaye ni Ndugu Hamisi Kiruri, mdogo wake kutoka Bunda Mkoa wa Mara. Karibuni sana wageni wa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: wanafunzi watano wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mbunge Justin Lazaro Nyamoga, ambao ni wageni, Wanakwaya wa Mtakatifu Don Bosco kutoka Kilolo, Mkoani Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vile vile wanafunzi 150 na Walimu 10 wa Shule ya Awali na Msingi *Mission* Kitunda kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Kitunda. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 45 na Walimu saba wa Shule ya Awali na Msingi *St. Gemma Galgan* kutoka Kondoa Mkoani Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Kondoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo lingine ambalo siyo la wageni. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la 2024, pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19 Mei, 2025, imewekwa kwenye vishikwambi kwa ajili ya rejea.

Baada ya matangazo hayo, sasa Katibu tuendelee.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, ili atoe maelezo kuhusu Muswada husika na aweze kutoa hoja kwamba sasa Muswada huo usomwe kwa mara ya pili, karibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutajalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 202)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea

kuiongoza Nchi kwa umahiri, mafanikio makubwa na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge Duniani *(IPU)* na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanahusu jina la Muswada. Sehemu ya Pili inapendekeza maboresho katika vifungu mbalimbali ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu mapya na kuboresha majukumu yaliyopo ya Bodi ya Shirika ambayo imekuwa ikiyatekeleza, lakini yalikuwa hayajabainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza ufanisi wa usimamizi wa Shirika. Aidha, Kifungu cha 5A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Bodi kuunda Kamati mbalimbali zitakazosaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha utendaji wa bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa nyaraka ambazo Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimisha mamlaka ya kuzisaini kwa Maafisa Waandamizi wa Shirika. Kwa utaratibu wa sasa Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimisha mamlaka ya kusaini mikataba ya upangaji pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha ukamilishaji wa mikataba ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu vya 12 na 13 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa wajibu wa mwajiri kukata kiasi cha fedha ya kodi ya nyumba pamoja na faini ya kuchelewesha kodi kutoka kwenye mshahara wa wafanyakazi, ambao ni wapangaji wa Shirika. Kwa mujibu wa utaratibu unaopendekezwa waajiriwa watalipa kodi ya pango kama ambavyo wapangaji binafsi wanalipa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji wa moja kwa moja kwa mpangaji katika kulipa kodi ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi za nyumba za Shirika.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 15, 16 na 17 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza viwango vya adhabu vilivyopitwa na wakati kwa mtu atakayebainika kutoa siri za shirika, kutoa taarifa za uongo na kujipatia manufaa kwenye shirika au anayezuia wafanyakazi wa shirika kuingia kwenye nyumba kufanya ukaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha adhabu kutolewa kulingana na hali halisi ya thamani ya fedha na uzito wa makosa pamoja na athari za makosa hayo. Aidha, marekebisho haya yanalenga kuviwezesha vyombo vya utoaji haki kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mtu binafsi au kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka mamlaka ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kuwa ni Rais badala ya Waziri pamoja na kuboresha masharti ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika usimamizi wa Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kifungu kipya cha 18A kinapendekezwa kuongezwa ili kutenganisha masharti yanayohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika na ajira za maafisa na wafanyakazi wengine wa Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mpangilio bora wa masharti ya Sheria kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha posho na malipo mengine ya Bodi kufanyika kwa mujibu wa miongozo inayotolewa na mamlaka husika. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti hayo na taratibu na miongozo inayohusiana na posho na malipo ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa taratibu zinazohusu michango ya mifuko ya hifadhi ya jamii na pensheni za matibabu kwa kuwa taratibu hizo zimetolewa na kufafanuliwa katika sheria zinazohusu hifadhi ya jamii na bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya Bodi kukasimisha majukumu kwa mfanyakazi yeyote wa shirika na badala yake Bodi iweze kukasimisha mamlaka yake kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika pekee. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti mamlaka ya ukasimishaji ya shirika pamoja na kuongeza ufanisi wa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza ruzuku kama chanzo cha mapato ya shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha uwezo wa kifedha wa shirika kwa lengo la utekelezaji bora wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa mamlaka ya Bodi ya kudhamini mikopo ya Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya kifungu hicho na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134, ambayo inabainisha taratibu za upatikanaji wa mikopo na dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya 25 na 26 vinapendekezwa kufutwa ili kuondoa masharti yanayohusu Mfuko wa Dhamana na Mfuko Mkuu wa Akiba uliyoundwa chini ya Sheria hii kwa kuwa vifungu hivyo havijawahi kutumika na havina umuhimu kwa shughuli za shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utendaji wa Shirika na kuhakikisha uwiano kati ya sheria na mahitaji halisi ya kiutendaji. *NHC* haitoi dhamana kwa wawekezaji binafsi wa sekta ya ujenzi wa nyumba, hivyo Mfuko wa Dhamana hauna maana kivitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Bodi kuwekeza bila kuhitaji kupata idhini ya Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha shirika kuwekeza kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 kuhusu uwekezaji wa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa na kifungu cha 31A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuondoa rejea ya masharti yanayohusu mgongano wa maslahi yaliyo katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Lengo la marekebisho haya ni kuweka masharti bora ya utaratibu wa udhibiti wa masuala yanayohusiana na mgongano wa maslahi ili kuliwezesha shirika kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu ya jumla. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha adhabu kutolewa kulingana na hali halisi ya thamani ya fedha na uzito wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha masharti yanayohusu Bodi na taratibu zilizopo za usimamizi wa mashirika ya umma. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa utawala wa Bodi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Act, 2025 Bill, 2025)* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DEOGRATIUS J. NDEJEMBI (MB), WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA WA MWAKA 2025 (*THE NATIONAL HOUSING CORPORATION* (*AMENDMENT) BILL, 2025*) - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 (*The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)*

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mhe. *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa umahiri, mafanikio makubwa na uzalendo wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, kumpongeza Mhe. Naibu Spika na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mwenyekiti,

**Mhe. Timotheo Paul Mnzava** (Mb.) pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 (The National Housing Corporation (Amendment) Act, 2025 Bill, 2025) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanahusu jina la Muswada. Sehemu ya Pili inapendekeza maboresho katika vifungu mbalimbali ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295 kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu mapya na kuboresha majukumu yaliyopo ya Bodi ya Shirika ambayo imekuwa ikiyatekeleza lakini yalikuwa hayajabainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa usimamizi wa Shirika. Aidha, Kifungu cha 5A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Bodi kuunda kamati mbalimbali zitakazosaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utendaji wa Bodi.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa nyaraka ambazo Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimisha mamlaka ya kuzisaini kwa maafisa waandamizi wa Shirika.

Kwa utaratibu wa sasa Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimisha mamlaka ya kusaini mikataba ya upangaji pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha ukamilishaji wa mikataba ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 12 na 13 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa wajibu wa mwajiri kukata kiasi cha fedha ya kodi ya nyumba pamoja na faini ya

kuchelewesha kodi kutoka kwenye mshahara wa mfanyakazi, ambaye ni mpangaji wa Shirika.

Kwa mujibu wa utaratibu unaopendekezwa waajiriwa watalipa kodi ya pango kama ambavyo wapangaji binafsi wanalipa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji wa moja kwa moja kwa mpangaji katika kulipa kodi ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi za nyumba za Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 15, 16 na 17 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza viwango vya adhabu vilivyopitwa na wakati kwa mtu atakayebainika kutoa siri za shirika, kutoa taarifa za uongo na kujipatia manufaa kwenye shirika au anayezuia wafanyakazi wa shirika kuingia kwenye nyumba kufanya ukaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha adhabu kutolewa kulingana na hali halisi ya thamani ya fedha na uzito wa makosa pamoja na athari za makosa hayo. Aidha, marekebisho haya yanalenga kuviwezesha vyombo vya utoaji haki kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mtu binafsi au kampuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka mamlaka ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kuwa ni Rais badala ya Waziri pamoja na kuboresha masharti ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika usimamizi wa Shirika.

Aidha, kifungu kipya cha 18A kinapendekezwa kuongezwa ili kutenganisha masharti yanayohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika na ajira za maafisa na wafanyakazi wengine wa Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mpangilio bora wa masharti ya Sheria kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha posho na malipo mengine ya Bodi kufanyika kwa mujibu wa miongozo inayotolewa na mamlaka husika. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti hayo na taratibu na miongozo inayohusiana na posho na malipo ya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa taratibu zinazohusu michango ya mifuko ya hifadhi ya jamii na pensheni za matibabu kwa kuwa taratibu hizo zimetolewa na kufafanuliwa katika sheria zinazohusu hifadhi ya jamii na bima ya afya.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya Bodi kukasimisha majukumu kwa mfanyakazi yeyote wa Shirika na badala yake Bodi iweze kukasimisha mamlaka yake kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika pekee. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti mamlaka ya ukasimishaji ya Shirika pamoja na kuongeza ufanisi wa Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza ruzuku kama chanzo cha mapato ya Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha uwezo wa kifedha wa Shirika kwa lengo la utekelezaji bora wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa mamlaka ya Bodi ya kudhamini mikopo ya Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya kifungu hicho na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134, ambayo inabainisha taratibu za upatikanaji wa mikopo na dhamana ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, vifungu vya 25 na 26 vinapendekezwa kufutwa ili kuondoa masharti yanayohusu Mfuko wa Dhamana na Mfuko Mkuu wa Akiba uliyoundwa chini ya Sheria hii Kwa kuwa vifungu hivyo havijawahi kutumika na havina umuhimu kwa shughuli za Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utendaji wa Shirika na kuhakikisha uwiano kati ya sheria na mahitaji halisi ya kiutendaji. NHC haitoi dhamana kwa wawekezaji binafsi wa sekta ya ujenzi wa nyumba, hivyo Mfuko wa Dhamana hauna maana kivitendo.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Bodi kuwekeza bila kuhitaji kupata idhini ya Waziri.

Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha Shirika kuwekeza kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 kuhusu uwekezaji wa mashirika ya umma.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa na kifungu cha 31A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuondoa rejea ya masharti yanayohusu mgongano wa maslahi yaliyo katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Lengo la marekebisho haya ni kuweka masharti bora ya utaratibu wa udhibiti wa masuala yanayohusiana na mgongano wa maslahi ili kuliwezesha Shirika kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu ya jumla. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha adhabu kutolewa kulingana na hali halisi ya thamani ya fedha na uzito wa kosa.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha masharti yanayohusu Bodi na taratibu zilizopo za usimamizi wa mashirika ya umma. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa utawala wa Bodi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Act, 2025 Bill, 2025)* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deogratius Ndejembi hoja hii ya Muswada imeungwa mkono.

Tunaendelea sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili aweze kuja kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti Timotheo Paul Mnzava, karibu. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment)* Bill, 2025].

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ulisomwa mara ya kwanza tarehe 14 Februari, 2025 katika Kikao cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Nane. Baada ya hatua hiyo, Muswada ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kamati ilifanya kazi ya uchambuzi na kuandaa maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna Kamati Ilivyofanya kazi. Kamati ilianza kazi ya uchambuzi kwa kutumia njia zifuatazo:-

(i) Kufanya mapitio ya jumla ya maudhui ya Muswada ulioletwa kwenye Kamati tarehe 3 Machi, 2025;

(ii) Kupokea maelezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tarehe 4 Machi, 2025 kwa lengo la kupata sababu na mantiki ya mapendekezo ya kufanya marekebisho;

(iii) Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Bunge. Kazi hii ilifanyika tarehe 5 Machi, 2025 kwa lengo la kupata mtazamo wa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria;

(iv) Kufanya uchambuzi wa kina kwa kupitia kifungu kwa kifungu cha Muswada pamoja na maoni ya Wadau. Baada ya hatua hiyo, hoja zilizojitokeza zilikabidhiwa kwa Waziri ili kupata ufafanuzi kabla ya kujenga msimamo; na

(v) Kupokea ufafanuzi wa Waziri na kufanya tena uchambuzi wa kina ili kujiridhisha na mantiki, manufaa na umuhimu wa kufanya marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao yaliyochangia kuuboresha muswada huu. Kipekee ninaomba kutambua mchango wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) na Chama cha Wanasheria Tanganyika (*TLS*) ambao kwa pamoja imeisaidia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Muswada**.** Uchambuzi wa Muswada huu ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi sehemu hii inatoa ufafanuzi wa uchambuzi kwa kubainisha madhumuni, sababu na maudhui ya Muswada.

Mheshimiwa Mheshimiwa, aidha, uchambuzi uliofanyika ulijielekeza katika masuala ya jumla kuhusiana na maudhui, masharti, mpangilio na madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa na Serikali. Vilevile, Kamati ilitathmini masuala mahsusi ikiwemo utekelezaji masharti pamoja na masuala mengine katika kila ibara ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa maudhui ya Muswada**.** kutokana na maelezo ya Serikali, Kamati imebaini kwamba, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295 ili kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Sheria hiyo ilitungwa mwaka 1990 kwa madhumuni ya kuvunja Ofisi ya Msajili wa Majumba, kuunda upya Shirika la Nyumba na kuweka masharti yatakayoberesha utendaji kazi wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na lengo la marekebisho yanayopendekezwa, Kamati ilipitia jina refu la Muswada na sehemu ya madhumuni na sababu. Kwa kufanya hivyo, Kamati iliweza kuoanisha ahadi za Serikali kwa wananchi kuhusu misingi ya uendeshaji wa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* na masharti yanayorekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina refu linabainisha kuwa mapendekezo haya yanalenga kuweka masharti bora kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za shirika kwa ufanisi. Kwa msingi huo, Kamati ilitafakari kila kifungu ili kuona iwapo kinaboresha masharti ya utekelezaji wa majukumu ya shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu masharti ya Ibara mbalimbali za Muswada. Ili kutathmini maudhui na masharti kwa kila ibara, Kamati ilitafakari sababu na madhumuni yaliyoelezwa na mtoa hoja. Madhumuni ya kufanya hivyo, ni kupata mantiki ya kila ibara na kulingana na madhumuni ya jumla na mapendekeo ya marekebisho. Uchambuzi umeonesha mambo makuu mawili. Mambo hayo ni ubora wa vifungu vinavyopendekezwa ikilinganishwa na lengo la jumla na changamoto zinazojitokeza ikilinganishwa na dhima ya Bunge kutunga Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila Ibara, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo stahili ili kuboresha maudhui yake. Ninapenda kulijulisha Bunge kwamba, kwa sehemu kubwa, Serikali imefanyia kazi ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, kwa lengo la kufanya rejea na kumbukumbu ya Bunge lako Tukufu, ninaomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya ibara ambazo Kamati ilitoa ushauri wake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2 ya Muswada**.** Katika Ibara ya 2 ya Muswada, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 5(2) cha Sheria Kuu. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza majukumu na kuboresha majukumu ambayo Bodi imekuwa ikiyatekeleza, lakini hayakuwa yamebainishwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza kwamba, ibara hiyo iboreshwe kwa namna ambayo, Kifungu cha Sheria kitakuwa na sharti la kuitaka bodi kuzingatia sheria nyingine za nchi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 8 ya Muswada, Serikali inarekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza viwango vya adhabu ambavyo vimepitwa na wakati.

Mheshimiswa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kwamba, adhabu iliyowekwa kwa kampuni ni ndogo ukilinganisha na aina ya kosa linalowekwa na sheria na ukilinganisha na kosa hilo linapotendwa na mtu binafsi. Kwa muktadha huo, ili kuweka uwiano wa adhabu unaolingana na kosa hilo. Kamati inapendekeza kwamba adhabu kwa kampuni iwe ni faini isiyopungua shilingi milioni mbili, na isiyozidi shilingi milioni kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 10 ya Muswada, Serikali inarekebisha Kifungu cha 18 cha Sheria Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka masharti mahsusi ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ambayo hayakuwepo hapo awali. Kamati inapendekeza kwamba, ibara hiyo ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza muda wa uzoefu wa miaka mitano kama moja ya vigezo na masharti vya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika anakuwa na sifa na uzoefu stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 11 ya Muswada, Serikali inafanya marekebisho ya Kifungu cha 18 kwa kuongeza Kifungu Kipya cha 18A ili kutenganisha masharti yanayohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika na ajira za maafisa na wafanyakazi wengine wa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano, usawa na uwazi katika ajira za utumishi wa umma, Kamati inapendekeza kwamba Kifungu kipya kiweke

masharti ambayo yatalilazimu shirika kuzingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 22 ya Muswada. Ibara ya 22 ya Muswada inafanya marekebisho katika Jedwali la Sheria *(schedule)* ambalo limeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5(3) cha Sheria. Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa marekebisho yanayopendekezwa katika Jedwali hilo, Kamati imeshauri kufanya marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Katika Aya ya 6, Kamati inapendekeza kuboresha masharti kwa kuongeza kifo kuwa moja ya sababu za kukoma kwa ujumbe wa Bodi;

(b) Katika Aya ya 8, Kamati inapendekeza kuboresha aya hiyo kwa kuweka masharti ambayo yataendana na Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 12 wa Mwaka 2015 ambao unazitaka Taasisi za Serikali kufanya vikao vya Bodi katika maeneo ya Serikali; na

(c) Katika Aya ya 9, Kamati inapendekeza kuweka masharti yanayobainisha wazi idadi kamili ya wajumbe ili kupata akidi ya Kikao cha Bodi. Lengo la pendekezo hili ni kuondoa utata unaoweza kujitokeza iwapo itatumika akidi ya wajumbe walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika kwamba, mapendekezo hayo yanakamilisha ahadi ya Serikali kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025. Ibara ya 76(i), Ukurasa wa 122 ilitoa ahadi kwa wananchi kuhusu kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ili litekeleze miradi yake kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa maeneo hayo utasaidia Bunge kutunga sheria madhubuti inayokidhi mahitaji ya biashara katika Sekta ya Miliki. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilikubaliana na Kamati na kuandaa jedwali la marekebisho kwa ajili ya kujadiliwa na Bunge kwa pamoja na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, maoni na maelezo ya jumla. Lengo la Kamati ni kutoa maoni kuhusu Muswada ni ili kuliwezesha Bunge iwapo mapendekezo ya kutunga Sheria yanafaa, yana tija au hayafai na hayana tija. Uchambuzi unaofanyika unagusa sehemu zote za Muswada ikiwemo jina refu, ibara za Muswada na Sehemu ya Sababu na Maudhui. Kwa upande wa ibara zilizochambuliwa Serikali imefanyia kazi maoni na ushauri ambapo jedwali la marekebisho limeandaliwa na mtoa hoja kama ilivyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Baada ya kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi, sasa ninaomba kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(i) Desturi ya Serikali kusikiliza maoni ya Wabunge na kuyafanyia kazi ipasavyo kama alivyofanya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni jambo linalopaswa kuigwa. Kamati inampongeza Waziri Mheshimiwa Deogratius J. Ndejembi, kwa usikivu unaozingatia kukidhi matarajio ya wananchi kupitia kwa wawakilishi wao;

(ii) Maboresho ya Sheria kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Shirika la Nyumba yatakuwa na tija zaidi iwapo shirika litawezeshwa kwa kusimamiwa katika ukusanyaji wa madeni na utekelezaji wa miradi yake. Kamati inashauri Serikali na taasisi zake ambazo ni wapangaji katika nyumba za Shirika la Nyumba, zilipe madeni yote ili kuliwezesha Shirika kutimiza majukumu yake;

(iii) Maboresho ya Sheria yanayoendana na ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 -2025 ni jambo la kupongezwa na linafaa kuendana na utekelezaji kamili wa ahadi iliyotolewa kwa wananchi kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa mara nyingine tena ninaomba kuishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuleta

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka, 2025. Kwa namna ya pekee, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano mkubwa waliotoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe hao wakiongozwa na wewe mwenyewe ukiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu, tunawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano mkubwa ambao mmeutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu na tunawatakia kila la heri kwenye majukumu yaliyo mbele yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa taarifa hii Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Kwa kutambua mchango wa wajumbe, ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba pamoja na Wataalam mbalimbali wa Serikali kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Ufafanuzi huo na maelezo yao yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru watumishi wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge kwa uongozi thabiti na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote wa kuuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati kuhusu Hoja. Baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA, 2023 *[THE NATIONAL HOUSING CORPORATION (AMENDMENT) BILL, 2026]* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment)* Bill, 2025]. Uwasilishaji huu unafanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa mara ya kwanza tarehe 14 Februari, 2025 katika Kikao cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Nane. Baada ya hatua hiyo, Muswada ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Bunge. Kwa kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya kazi ya uchambuzi na kuandaa maoni yake.

#### 1.2 Namna Kamati Ilivyofanya kazi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza kazi ya uchambuzi kwa kutumia njia zifuatazo:-

(i) Kufanya mapitio ya jumla ya maudhui ya Muswada ulioletwa kwenye Kamati tarehe 03 Machi, 2025;

(ii) Kupokea maelezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tarehe 04 Machi, 2025 kwa lengo la kupata sababu na mantiki ya mapendekezo ya kufanya marekebisho;Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Bunge. Kazi hii ilifanyika tarehe 05 Machi, 2025 kwa lengo la kupata mtazamo wa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria;

(iii) Kufanya uchambuzi wa kina kwa kupitia kifungu kwa kifungu cha Muswada pamoja na maoni ya Wadau.

(iv) Baada ya hatua hiyo, hoja zilizojitokeza zilikabidhiwa kwa Waziri ili kupata ufafanuzi kabla ya kujenga msimamo; na

(v) Kupokea ufafanuzi wa Waziri na kufanya tena uchambuzi wa kina ili kujiridhisha na mantiki, manufaa na umuhimu wa kufanya marekebisho yanayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kuwashukuru wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao yaliyochangia kuuboresha muswada huu. Kipekee naomba kutambua mchango wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ambao kwa pamoja imeisaidia Kamati.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Muswada huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi sehemu hii imetoa

ufafanuzi wa uchambuzi kwa kubainisha madhumuni, sababu na maudhui ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, uchambuzi uliofanyika ulijielekeza katika masuala ya jumla kuhusiana na maudhui, masharti, mpangilio na madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa na Serikali. Vilevile, Kamati ilitathmini masuala mahsusi ikiwemo utekelezaji masharti *(practicability)* pamoja na masuala mengine katika kila ibara ya Muswada.

### 2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na maelezo ya Serikali, Kamati imebaini kwamba, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295 ili kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Sheria hiyo ilitungwa mwaka 1990 kwa madhumuni ya kuvunja Ofisi ya Msajili wa Majumba, kuunda upya Shirika la Nyumba na kuweka masharti yatakayoberesha utendaji wa Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na lengo la marekebisho yanayopendekezwa, Kamati ilipitia jina refu la Muswada na sehemu ya madhumuni na sababu. Kwa kufanya hivyo, Kamati iliweza kuoanisha ahadi za Serikali kwa wananchi kuhusu misingi ya uendeshaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na masharti yanayorekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, jina refu linabainisha kuwa mapendekezo haya yanalenga kuweka masharti bora kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Shirika kwa ufanisi. Kwa msingi huo, Kamati ilitafakari kila kifungu ili kuona iwapo kinaboresha masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika.

### 2.3 Uchambuzi Kuhusu Masharti ya Ibara Mbalimbali za Muswada

**Mheshimiwa Spika,** ili kutathmini maudhui na masharti kwa kila ibara, Kamati ilitafakari sababu na madhumuni yaliyoelezwa na mtoa hoja. Madhumuni ya kufanya hivyo, ni kupata mantiki ya

kila ibara na kulinganisha na madhumuni ya jumla ya mapendekeo ya marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha mambo makuu mawili. Mambo hayo ni ubora wa vifungu vinavyopendekezwa ikilinganishwa na lengo la jumla na changamoto zinazojitokeza ikilinganishwa na dhima ya Bunge kutunga Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, katika kila Ibara, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo stahili ili kuboresha maudhui yake. Napenda kulijulisha Bunge kwamba, kwa sehemu kubwa, Serikali imeyafanyia kazi ushauri na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kwa lengo la kufanya rejea na kumbukumbu ya Bunge lako Tukufu, naomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya ibara ambazo Kamati ilitoa ushauri wake kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Ibara ya 2 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 2 ya Muswada, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 5 (2) cha Sheria Kuu *(Principal Act)*. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza majukumu na kuboresha majukumu ambayo Bodi imekuwa ikiyatekeleza lakini hayakubainishwa na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipendekeza kwamba, Ibara hiyo iboreshwe kwa namna ambayo, Kifungu cha Sheria kitakuwa na sharti la kuitaka bodi kuzingatia Sheria nyingine za nchi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Pendekezo hili lina lengo la kuhakikisha kwamba, Bodi inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mawanda ya sheria mbalimbali za nchi.

### 2.3.2 Ibara ya 8 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 8, Serikali inarekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza viwango vya adhabu ambavyo vimepitwa na wakati.

**Mheshimiswa Spika**, Kamati ina maoni kwamba, adhabu iliyowekwa kwa kampuni ni ndogo ukilinganisha na aina ya kosa linalowekwa na sheria ukilinganisha na kosa hilo linapotendwa na mtu binafsi. Kwa muktadha huo, ili kuweka uwiano wa adhabu unaolingana na kosa hilo, Kamati inapendekeza kwamba adhabu kwa kampuni iwe ni faini isiyopungua shilingi milioni mbili, na isiyozidi shilingi milioni kumi.

### 2.3.3 Ibara ya 10 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 10, Serikali inarekebisha Kifungu cha 18 cha Sheria Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka masharti mahsusi ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ambayo hayakuwepo hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, Ibara hiyo ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza muda wa uzoefu wa miaka mitano (5) kama moja ya vigezo na masharti vya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika anakuwa na sifa na uzoefu stahiki.

### 2.3.4 Ibara ya 11 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 11, Serikali inafanya marekebisho ya Kifungu cha 18 kwa kuongeza Kifungu Kipya cha 18A ili kutenganisha masharti yanayohusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika na ajira za maafisa na wafanyakazi wengine wa Shirika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano, usawa na uwazi katika ajira za utumishi wa umma, Kamati inapendekeza kwamba Kifungu kipya kiweke masharti ambayo yatalilazimu Shirika kuzingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma.[1]

[1] Sura ya 298

### 2.3.5 Ibara ya 22 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 22 ya Muswada inafanya marekebisho katika Jedwali la Sheria *(schedule)* ambalo limeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (3) cha Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa marekebisho yanayopendekezwa katika Jedwali hilo, Kamati imeshauri kufanya marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Katika **Aya ya 6**, Kamati inapendekeza kuboresha masharti kwa kuongeza tukio la kifo kuwa moja ya sababu za kukoma kwa ujumbe wa Bodi;

(b) Katika **Aya ya 8**, Kamati inapendekeza kuboresha aya hiyo kwa kuweka masharti ambayo yataendana na Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 12 wa Mwaka 2015 ambao unazitaka Taasisi za Serikali kufanya vikao vya Bodi katika maeneo ya Serikali; na

(c) Katika **Aya ya 9**, Kamati inapendekeza kuweka masharti yanayobainisha wazi idadi kamili ya wajumbe ili kupata akidi ya Kikao cha Bodi. Lengo la pendekezo hili ni kuondoa utata unaoweza kujitokeza iwapo litatumika akidi ya wajumbe walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika kwamba, mapendekezo hayo yanakamilisha ahadi ya Serikali kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025. Ibara ya 76 (i) Uk. 122 ilitoa ahadi kwa wananchi kuhusu kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili litekeleze miradi yake kwa tija.

**Mheshimiwa Spika,** uboreshaji wa maeneo hayo utasaidia Bunge kutunga Sheria madhubuti inayokidhi mahitaji ya biashara katika sekta ya Miliki. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilikubaliana na Kamati na kuandaa jedwali la marekebisho kwa ajili ya kujadiliwa na Bunge kwa pamoja na muswada huu.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la Kamati ni kutoa maoni kuhusu Muswada ni kuliwezesha Bunge iwapo mapendekezo ya kutunga Sheria yanafaa, yanatija au hayafai na hayana tija. Uchambuzi unaofanyika unagusa sehemu zote za Muswada ikiwemo jina refu,Ibara na sehemu ya Sababu na madhumuni. Kwa upande wa Ibara zilizochambuliwa Serikali imefanyia kazi maoni na ushauri ambapo Jedwali la Marekebisho limeandaliwa na mtoa Hoja kama ilivyoshauriwa na Kamati.

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi, sasa naomba kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(a) Desturi ya Serikali kusikiliza maoni ya wabunge na kuyafanyia kazi ipasavyo kama ilivyofanya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni jambo linalopaswa kuigwa na Wizara zote. Kamati inampongeza Waziri Mhe. Deogratius J. Ndejembi, Mb kwa usikivu unaozingatia kukidhi matarajio ya wananchi kupitia kwa wawakilishi wao;

(b) Maboresho ya Sheria kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Shirika la Nyumba yatakuwa na tija zaidi iwapo Shirika litawezeshwa kwa kusimamiwa katika ukusanyaji wa madeni na utekelezaji wa miradi yake. Kamati inashauri Serikali na taasisi zake ambazo ni wapangaji katika nyumba za Shirika zilipe madeni yote ili liweze kufanya kazi inavyostahili;

(c) Maboresho ya Sheria yanayoendana na ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 -2025 ni jambo la kupongezwa na linafaa kuendana na utekelezaji kamili

wa ahadi iliyotolewa kwa wananchi kuhusu ujenzi wa nyumba 1000 za gharama nafuu jijini Dodoma. Kamati inashauri kuwa, Shirika la Nyumba la Taifa liendelee na mradi wa ujenzi wa nyumba hizo kwa kuzingatia masharti ya marekebisho ya Sheria hii.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba kukushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka, 2025 kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwa namna ya pekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Aidha, weledi na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha ukamilifu wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naamini kwa taarifa hii Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Kwa kutambua mchango wa Wajumbe, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni kama yafuatayo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Timotheo P. Mnzava, Mb | | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb | | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Innocent Bilakwate, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | - | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Festo Richard Sanga, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Shaban Omari Shekilindi, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Asha Juma Abdallah, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Ufafanuzi huo na maelezo yao yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa uongozi wake thabiti wa kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Timotheo P. Mnzava, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
09 Juni,2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza kuchangia, ninaanza na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, baadaye atafuata Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu ambao upo mbele yetu. Kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kuleta Muswada huu na mabadiliko haya ambayo sisi kama Kamati tumeyapitia na tumeona ni vitu ambavyo vina maslahi kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pia nimpongeze Katibu Mkuu, kaka yangu Anthony Sanga kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Tangu ameingia Wizara hii tumeona mapinduzi *(revolution)* akiyafanya na mojawapo ni vitu kama hivi ambavyo vina maslahi mapana kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nizungumze mambo machache. Kwanza, niunge mkono hoja, mabadiliko yote sisi Kamati ambayo tumeyapendekeza. Pia, ninapongeza kwa sababu haya pia yanaenda kuungana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025-2030, ukurasa namba 26 ambao umejikita katika kuelezea namna gani Serikali imejipanga katika kuboresha eneo la makazi na *real estate* kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mawazo yangu yatakuwa kwenye Ibara ya 18 kwa maana ya uteuzi wa Rais wa Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing*. Sisi kama Kamati tumeliona hili ni jambo kubwa sana, kwanza kwa sababu linakuwa linaweka *check and balance* ndani ya Wizara kwa maana Waziri hausiki kabisa kwenye uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Pili, tunafanya shirika hili liwe huru kwenye utendaji kazi wake usiweze kuingiliwa kimaamuzi na Waziri labda kwa uhitaji husika lakini siyo kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ambazo tumezianisha hapa za kuhakikisha kwamba Mkurugenzi Mkuu anayeteuliwa angalau ni Mkurugenzi ambaye ana uzoevu ambao unaendana na maeneo ya *real estate* lakini sekta ya ardhi, mambo ya sheria pia ni mtu ambaye anajua mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivi ili kuhakikisha kwamba, tunapata Mkurugenzi ambaye ni *aggressive* kutokana kwamba, sekta hii ya *real estate* au sekta hii ya ujenzi kwenye Shirika kama la *National Housing* inahitaji mtu ambaye yuko *current,* mtu ambaye pia anaweza kupambana na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuunga mkono maoni haya na kwamba, sasa ni fursa nzuri tunaenda kupata viongozi ambao watakuwa na tija. Tunaamini pia, hata Mkurugenzi ambaye tuko naye sasa hivi anafanya kazi kubwa sana na ni nzuri sana na ni mtu ambaye kwa kweli tangu ameingia kwenye shirika hili tunaona mapinduzi *(revolution)* kwamba shirika lina vitu ambavyo inavifanya kwenye utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwenye Vifungu vya 15, 16 na 17 ambapo, kwa kweli tuliona kwamba hapo nyuma kulikuwepo na *loophole*. Kulikuwa na nafasi mtu anaweza akatumia Shirika kwa mfano, kwenye vitu kama vya kwenye *joint venture* akaenda akalidanganya shirika akatoa taarifa za uwongo na baadaye shirika likaingia hasara, kwa sababu muda mwingi kuna watu wanatumia fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu kama *National Housing* lina maeneo mengi ambayo ni *potential* kwenye nchi yetu, maeneo ya miji pia maeneo yenye masoko makubwa. Kwa hiyo, watu wengine wanatumia taarifa ambazo siyo sahihi kwamba wanamitaji na kadhalika ili waingie u-*joint venture* na shirika na mwisho wanafanya shirika letu linaingia hasara kwa sababu wanakuwa hawana uwezo wa hicho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuweka utaratibu huu wa faini kuhakikisha kwamba mtu yeyote ambaye anahusika kwenye

kudanganya eneo hili tunamtoza faini na tunamtia hatiani, ni jambo zuri sana ili kuhakikisha kwamba hawa matapeli na watu ambao wanaweza kuliharibia sifa za shirika na kukwamisha malengo ya shirika wanachukuliwa hatua. Kwa hiyo, nilipongeze na niunge mkono hoja maoni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwenye suala la majukumu ya kwenye vikao vya bodi. Sisi kama Kamati tuliliona hili kwamba bodi inaweza ikawa na vikao vyake inavyotaka kuvifanya lakini vikao hivi kama mtu siyo mwaminifu anaweza akaamua kikao kingine akaitisha kikaenda kufanyika China na anaenda kupitisha eneo lingine. Sasa Kamati tuliliona hili kwenye Ibara ya 22 aya Na.8, tuliangalia kwamba ni muhimu sasa Bodi inapotaka kufanya vikao iangalie Waraka wa Msajili wa Hazina, ambao unaelekeza kwamba vikao vyote vifanyike ndani ya Serikali yetu, ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kitu ambacho tunafanya haya ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na yale ambayo nyuma yalikuwepo ya kwamba, Bodi inaenda kufanya vikao nje ya nchi ambapo baadaye imekuwa ikipigiwa kelele kwamba pia inatia hasara na inatia walakini kwenye utendaji kazi. Kwa hiyo, hiki ni kitu kikubwa kwetu kama Kamati kwamba, Bodi inapotaka kufanya vikao ni lazima izingatie Waraka wa Msajili wa Hazina ambao pia waraka huo unaelekeza kwamba haya yafanyike ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunaunga mkono hoja kwenye suala hilo pia la marekebisho ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kama Mjumbe wa Kamati, tunatamani sana Wabunge wenzetu pia watuunge mkono kwenye maoni haya ili liweze kutekelezwa na tuiruhusu sasa Wizara na *National Housing* waende wakafanye kazi. Maoni haya yamekuwa ni maoni jumuishi, ni maoni ambayo kwa kweli yamezingatia sana kuhakikisha kwamba sekta hii ni sekta ambayo inakua kwa kasi, kwa hiyo ni lazima kuna mabadiliko ambayo lazima yaendana na wakati wa sasa. Kwa hiyo, Kamati tunatamani kuomba pia wadau, Wabunge wenzetu watuunge mkono kuhusu hili jambo liweze kupitishwa na liweze likasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme ninaunga mkono hoja na ninamtakia kila kheri Mheshimiwa Waziri na ninawatakia kila la heri *National Housing,* tukiamini kabisa kwamba wanaenda kuwa *aggressive* kwenye soko, lakini pia wanaenda kuhakikisha kwamba wanaenda kufanya mabadiliko yale ambayo Chama Cha Mapinduzi kimefanya kwenye Mkutano Mkuu na kuelekeza kwamba kwenye Ilani ya Mwaka 2025/2030 kinaenda kuboresha makazi ya watu, kinaenda kuboresha upatikanaji wa nyumba nafuu, upatikanaji wa nyumba ambazo ni Watanzania wengi ambao wana uhitaji wa nyumba hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatamani yale maeneo ambayo yamekuwa yakikaa muda mrefu au nyumba za *National Housing* ziko muda mrefu hazifanyi kazi, hasa kupitia mabadiliko haya wataenda kufanya shirika hili ni shirika kinara na kwa sababu pia *National Housing* inaendeshwa kibiashara, tunatamani sana kwamba shirika letu liweze kufanya kazi na ndiyo maana kuna maeneo ya Ibara hapa tumeweza kufanya mabadiliko kwamba uwekezaji kwenye Bodi usimsubirie Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivi ni kwa sababu Waziri anaweza akatengeneza *bureaucracy,* Bodi wakati inaona kwamba soko sasa linahitajika hadi ikamwandikie Waziri, Waziri aje akarudishe mchakato huo siyo leo inawezekana hilo soko ni la kwanza limepitwa na wakati. Ndiyo maana kwenye mabadiliko hapa tumeruhusu Bodi ifanye uwekezaji bila kufanya *consultation* kwa Mheshimiwa Waziri ili Bodi iwe *aggressive* kwenye matumizi yake na uamuzi huo ambao inaufanya kutokana na hitaji la soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kupunguza *bureaucracy* kwenye maamuzi ambayo shirika linataka kuyafanya ambao kwa sababu linajiendesha kibiashara ni lazima liendane na wakati ni lazima liendane na soko na ndiyo maana tunatengeneza mazingira yote kuhakikisha kwamba sasa visingizio kwenye *National Housing* vitakuwa havipo, kwa sababu watakuwa na maamuzi huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatakie kila la heri watumishi wa *National Housing* na ninaitakia kila la heri Wizara yetu kuhakikisha kwamba tunafanikisha hili pia tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kazi kubwa aliyoikusudia ya kubadilisha sekta ya ardhi nchini, hususan kwenye *real estate* ambayo kwa Taifa letu *National Housing* wanayo nafasi kubwa kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja maoni ya Kamati yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ahsante sana kwa mchango wako huo ambao umebainisha faida za Muswada huu.

Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii adhimu na muhimu ambayo leo nasimama hapa *insha Allah* pengine itakuwa siyo mara mwisho kwa sababu sifa zote ninazo, uwezo ninao, akili yangu iko timamu. Ninashukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia huu Muswada wa Marekebisho ya Shirika la Nyumba la Taifa ambao umekuja wakati muafaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mungu pia kwa kibali hicho cha afya njema aliyonijalia leo kusimama hapa madhubuti kwa lengo la kutekeleza moja katika jukumu langu ambalo ni kuiwakilisha Kamati yangu ambayo naihudumu. Kabla sijaendelea sana heshima ya kipekee nampongeza sana Jemedari wetu, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake njema aliyonayo katika ujenzi na uongozi wake kwa kweli ninathubutu kusema Rais Dkt. Samia ameweza na ameweza sana, semeni ndiyo! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umahiri wake na uhodari wake ni waziwazi, tutaendelea

kumuunga mkono kwa bidii zetu zote na kuhakikisha siku hiyo inafika mitano tena inamsubiria mapemaaa asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kwanza niendelee kutoa pongezi nyingine kwa Waziri Mheshimiwa Deo na Naibu Waziri Mheshimiwa Pinda. Viongozi hawa wameonesha weledi wa hali ya juu. Katibu Mkuu Ndugu Anthony Sanga naye hakubaki nyuma na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Lucy, viongozi hawa wame-*demonstrate* uongozi wa namna ya kipekee, sikumsahau mhusika wa leo Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing* Ndugu Hamad Abdallah, ambaye pamoja na Watendaji wake wameweza kufanya kazi nzuri sana kulisimamia Shirika la Nyumba la Taifa mpaka leo hali inaonekana hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania yetu imekuwa na majengo ya kileo sana, kwa mfano Samia *Complex* kule Msasani kule Kawe, Morocco *Square* utafikiri uko 'LA', utadhani uko Los Angeles, nchi yetu inakwenda kubadilika sana. Kwa hivyo, ni wakati muafaka kuleta huu Muswada kuipa nguvu sana *National Housing* ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ustawi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nigusie Kifungu cha 5, ambacho kimeeleza majukumu ya Bodi. Huko nyuma Bodi imekuwa ikitekeleza majukumu mbalimbali, lakini hayakuwa yametamkwa na sheria, kwa Muswada huu sasa majukumu ya Bodi yatakuwa rasmi na kwa mujibu wa sheria, kwa hivyo yanawapa na tunatoa nguvu zaidi kwa Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kugusia uwezo wa Bodi kuamua juu ya wawekezaji. Huko nyuma, sheria ilikuwa inalazimisha kwamba ili Bodi iweze kuwekeza ilikuwa inahitaji kibali cha Waziri, jambo ambalo Mheshimiwa Festo amelikazania sana hapa. Jambo ambalo lilikuwa gumu kwani Waziri hana wataalam wa mambo hayo ya kibiashara. Kwa hivyo Kifungu hichi cha 27 kinaipa Bodi nguvu ya kuwekeza bila kibali cha Waziri kwa kuangalia sababu za kibiashara na kwa hivyo kupunguza ukiritimba na *bureaucracy*. Kwa hivyo, kwa kuweka nafasi hii mambo ya uwekezaji yatakuwa yanafanyika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia uamuzi juu ya mikopo. Sheria ya awali ilikuwa inaipa Bodi ya Wakurugenzi nguvu na mamlaka ya kudhamini mikopo ya shirika, wakati kwa sasa Serikali inayo sheria mahsusi inayosimamia mikopo kwa taasisi na mashirika ya umma. Sheria hii linaondoa mkanganyiko huo kwa kuondoa mamlaka hayo kwa bodi ili shirika likope kwa mujibu wa sheria inayosimamia mikopo yote ya Serikali jambo ambalo lina tija zaidi, Kifungu Na. 24 kinafuta Mamlaka ya Bodi kudhamini mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumzie juu ya ajira kwa Watumishi wa Serikali. Kifungu cha 18A kinaipa Bodi mamlaka ya kuajiri na kusimamia ajira za watumishi wa shirika. Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kukubaliana na Kamati kwa mamlaka haya ya bodi yafanyike kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, maboresho haya ni muhimu sana kwa ustawi na ufanisi wa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maboresho ya sheria hii tunaenda kuipa nguvu sana Shirika la Nyumba utekelezaji wa kazi zake na sisi wenyewe tunategemea kwamba hii ni moja katika utekelezaji wa Ilani kwa hivyo hatuna sababu tusipewe mitano tena na Rais Dkt. Samia akawa ndiye Rais, tena Rais Mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nani kama Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii ahsante sana na ninawaomba wananchi wanaoniona kule Zanzibar wanifikirie na mimi mitano tena inanihusu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, ahsante sana.

Ninamwita sasa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu kutuweka katika usalama wa

mikono yake na leo tumesimama hapa kwa ajili ya wasilisho la mapendekezo ya Sheria hii ya *National Housing.* Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwangu binafsi kwa kweli kwa kuendelea kuniamini kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kipindi changu chote ambacho nimefanya kazi za Ubunge, nimekuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na sasa niko ninasaidiana na Mheshimiwa Waziri hapa wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Kavuu na niliposimama hapa maana yake ninawaambia jamani nipo na kazi lazima iendelee na niliwaambia tuna miaka mitano ya kazi na Mheshimiwa Mama Samia ameniunga mkono sana, mambo yaliyofanyika kule ni makubwa sana, ninaamini wanaamini jembe lao lipo na tutaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote ninashukuru maoni ya Waheshimiwa Wabunge wawili waliopata nafasi ya kuchangia, kwa kweli wanaungana nasi katika pendekezo hili. Kwa sababu ya uchache wa wachangiaji maana yake jambo hili limekubalika na Waheshimiwa Wabunge wote na kwa sasa nina uhakika kabisa watakapokwenda kwenye mjadala wanaenda kutusaidia kutuidhinishia hili suala ambalo ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu na hasa kwa Shirika la kibiashara kama *National Housing* ambalo kimsingi linakanyaga kwenye miguu ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri watu wa Chamwino, kule watambue uwepo wako wasichezee shilingi waliyonayo mkononi, chako ulichokula hicho kingine hicho ni njaa tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wangu ninamkushukuru sana amekuwa msaada mkubwa kwangu katika kutekeleza wajibu ambao amenipangia majukumu yake na leo ninaingia kwenye Historia ya Utungaji wa Sheria ya *National Housing* katika mabadiliko yake ya kuelekea kwenye dunia mpya ya uchumi wa kiteknolojia kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe msemaji wa mambo mengi nimwachie Mheshimiwa Waziri akafanye majumuisho lakini kwa ujumla wake ninatoa shukrani nyingi sana. Ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo hayo.

Sasa ninamkaribisha mtoa hoja, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili aweze kuhitimisha hoja yake, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nichukue nafasi hii tena kukushukuru wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kuweza kusimama hapa leo na kuleta Muswada huu mbele ya Bunge hili. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wachangiaji Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Asha Mshua ambao ninawahakikishia kwamba yale waliyoyasema tutayazingatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru pia tena kipekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa maoni waliyoyatoa, ushauri hasa katika kipindi ambacho tulikuwa tunapitia huu Muswada wa Sheria na ninakushukuru wewe kama Makamu Mwenyekiti vilevile wa hii Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho haya ambayo yanaenda kufanyika yanakwenda kurahisisha *decision-making process* katika utendaji wa *day to day* wa Shirika la Nyumba la Taifa. Katika kufanya hivyo maana yake mlaji wa mwisho ambaye ni mwananchi anakwenda kupata huduma iliyobora. Maamuzi ya uwekezaji, maamuzi ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu, maamuzi ya kuhakikisha ya kwamba tunaweka miji yetu kwa ujenzi wa kwenda juu kupitia Shirika letu la Nyumba la Taifa yote yanakwenda kufanyika kwa haraka zaidi kwa mabadiliko ya sheria hizi. Kwa hiyo, ninawashukuru sana na ningeomba

Wabunge waridhie baadaye tunapopitisha, basi sheria hii iweze kupita ili tuweze kwenda kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Hoja imeungwa mkono, sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Sasa nimwite, Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1) ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Taifa la Nyumba wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono na sasa nitalihoji Bunge kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)*. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BAKARI KISOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa Sura ya 1995, kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo yamebainika wakati wa Utekelezaji wa Sheria hiyo *(A Bill for an Act to Amend the National Housing Corporation Act, in order to keep the Law updated with some Challenges Observed in its Implementations)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 (The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025) Ulipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukamilisha taratibu zote za kupitisha Muswada huu na kusomwa kwa mara ya tatu, sasa ninatangaza rasmi kwamba, Muswada huu Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa la Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)* sasa umepitishwa na Bunge rasmi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitisha Muswada huu ninaamini sasa taratibu zitakazofuata ni kwa mujibu wa Katiba Mheshimiwa Rais kwenda kuusaini Muswada huu ambao ni sheria sasa ili kazi sasa ziweze kufanyika. Kwa hiyo, nami nitumie fursa hii sana kuipongeza Serikali yote kwa ujumla chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anasimamia masuala yetu ya nyumba na makazi katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu, Deogratius Ndejembi, Naibu Waziri wake Geophrey Mizengo Pinda, lakini na Watendaji Wakuu akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na mhusika mkuu mwenyewe Mkurugenzi Mkuu wa Shirika letu la Nyumba. Kwa kweli, Muswada huu umepita kwa namna ambayo inadhihirisha wazi kwamba wadau wote wameridhika, lakini na Bunge letu limeridhia kwa sabau Serikali imeshaurika vizuri na Kamati imeifanya kazi kama ambavyo Bunge linatakiwa lifanye.

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwatakie kila la kheri nikiamini kwamba, sasa hivi Shirika letu la Nyumba linakwenda kujiendesha kibiashara na kwa mujibu wa marekebisho haya ya sheria shirika letu litakuwa na manufaa zaidi kwa Watanzania lakini na mambo mengine ya kibiashara kwa Serikali yatapata faida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninawashukuru sana na ninawatakia mchana mwema kwa siku hii ya leo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 5.23 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 10 Juni, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*